Nipashe
Jumatatu Juni 27, 2022 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-
ISSN 0856 • Na. 0580989
www.ippmedia.com
MWANGA WA JAMII
www.twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper
LIKE & FOLLOW US




**YANGA YAITEKA DAR, MAPOKEZI YAKE NI KUFURU, BARABARA ZAFUNGWA**
UKURASA 24

SportPesa
JACKPOT BABA LAO!
TZS. 267,714,020
CHEZA SASA KWA 1000/= TU!
SPORTPESA.CO.TZ | PIGA *150*87#



**Biashara** kuazima 'mawigi' ilivyoshamiri, daktari ataja madhara
UKURASA 4



# Maagizo 10 serikali ikitoa maelfu ya ajira Afya, Elimu
UKURASA 2

UKURASA WA 4
**WAZIRI UMMY ATOA SOMO KUEPUKA KUZAA WATOTO WENYE VICHWA VIKUBWA**

## PM: Serikali kuendelea kuheshimu mchango taasisi za dini
UKURASA 3



Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, akimpongeza Askofu Wolfgang John Pisa baada ya kusimikwa kuwa Askofu wa Jimbo Katoliki la Lindi katika ibada iiyofanyika Uwanja wa Ilulu mjini Lindi jana. **PICHA: OFISI YA WAZIRI MKUU**

Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Hemed Suleiman Abdulla, akizindua huduma ya Go na NMB katika tamasha lililofanyika Zanzibar mwishoni mwa wiki. Watatu kulia ni Ofisa Mtendaji Mkuu wa NMB, Ruth Zaipuna, Ofisa Mkuu wa Biashara na Wateja Binafsi, Filbert Mponzi (wapili kulia) na Meneja wa Biashara wa Benki ya NMB Zanzibar, Naima Said Shaame, kushoto ni Mkuu wa Wilaya ya Mjini, Rashid Simai Msaraka. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**




## Madudu gari la serikali lauzwa mil. 4/- limetembea kilomita 900
UKURASA 2

MICHEZO SIMBA YATESEKA KWA PRISONS UK.24 MAONI, KATUNI UK.6



Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Dk. Angeline Mabula, akizungumza katika mkutano wa wadau wa uandaaji, utekelezaji na usimamizi wa mipango ya matumizi ya ardhi Halmashauri ya Wilaya ya Nzega mkoani Tabora hivi karibuni. Wapili kushoto ni Mkuu wa Mkoa wa Tabora, Balozi Dk. Batilda Salha Burian. **PICHA: MPIGAPICHA**

# Maagizo 10 serikali ikitoa maelfu ya ajira Afya, Elimu

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Innocent Bashungwa, ametoa maagizo 10 kwa waajiri na waajiriwa wapya wa ajira za afya na ualimu ikiwamo wasioripoti kwa muda uliopangwa nafasi zao zitachukuliwa na kupewa wengine.

Pia waajiri wote kuhakikisha wanapokea vyeti na kuviwasilisha Baraza la Mitihani Tanzania (NECTA) kwa ajili ya uhakiki na watakaokutwa na vyeti vya kugushi hatua kali zichukuliwe.

Bashungwa alitoa maagizo hayo jana jijini hapo alipokuwa akitangaza walioajiriwa kwenye kada ya afya na ualimu 16,676.

Alitaka waajiriwa wapya wote kuripoti kwa wakurugenzi wa halmashauri walizopangiwa wakiwa na Kitambulisho cha Taifa au namba ya utambulisho ya NIDA, cheti halisi cha kuzaliwa, vyeti halisi vyote vya taaluma na utaalamu wa kazi vya mwajiriwa, ili vihakikiwe na mwajiri kabla ya kupewa barua ya ajira.

"Waajiri wote wanapokea vyeti waviwasilishe baraza la mitihani kwa ajili ya uhakiki. Wizara ipewe taarifa mara moja kwa wale watakaokutwa na vyeti ambavyo ni vya kughushi ili hatua kali zichukuliwe," aliagiza.

Katika maagizo hayo waajiri wote wametakiwa kuhakikisha watumishi wapya waliopangwa kwenye halmashauri, wanapewa barua za ajira, na kuripoti kwenye vituo walivyopangiwa na sio vinginevyo.

"Mwajiriwa mpya atakayechukua posho ya kujikimu, na baadaye asiripoti katika kituo chake cha kazi alichopangiwa, atachukuliwa hatua stahiki kwa mujibu wa sheria," alionya Bashungwa.

Pia, aliwaagiza waajiriwa wapya watakaoshindwa kuripoti katika vituo walivyopangiwa ndani ya siku 14, kuanzia leo watakuwa wamepoteza nafasi zao na zitajazwa na waombaji wengine wenye sifa waliopo kwenye Kanzidata ya Ofisi ya Rais - TAMISEMI.

"Wakurugenzi wa Mamlaka za Serikali za Mitaa ambazo waajiriwa wapya wamepangwa, wawapokee na kuwawezesha kwa kuzingatia sheria, kanuni, taratibu na miongozo ya utumishi wa umma, na baadaye kutoa taarifa ya kuripoti kwao," alisema. Alisisitiza taarifa za kuripoti waajiriwa hao zijazwe kwenye mfumo wa kielektroniki (ajira.tamisemi.go.tz), baada ya kila mtumishi kupokelewa na kukamilisha taratibu.

"Wakurugenzi wa Mamlaka za Serikali za Mitaa wanaelekezwa kukamilisha taratibu za ajira haraka, ili waajiriwa wapya waingizwe kwenye mfumo wa taarifa za kiutumishi na mishahara (HCMIS) mapema iwezekanavyo." Aliagiza Makatibu Tawala wa Mikoa na Wakurugenzi wote wa Halmashauri, kutekeleza maagizo ya OR-TAMISEMI yaliyotolewa mwezi Machi, 2022 ya kufanya msawazo wa Ikama ya walimu wa shule za msingi na sekondari, ndani ya mkoa na halmashauri kabla au ifikapo Juni 30, 2022.

"Tekelezeni kwa bidii maelekezo hayo ili shule zinakuwa na uwiano mzuri wa walimu, na taarifa ya utekelezaji iwasilishwe kabla au ifikapo tarehe 15 Julai, 2022. OR-TAMISEMI haitasita kumchukulia hatua mwajiri ambaye hatatekeleza maelekezo haya ya kufanya msawazo wa walimu katika kuleta uwiano wa mwalimu na wanafunzi wa 1:60 ulioelekezwa," alisema.

Kadhalika, alisema ameelekeza wakuu wa shule na walimu wakuu kushirikiana na bodi zao za shule ili kufuata miongozo ambayo wizara imetoa kwa ajili ya michango ya wanafunzi wanaoendelea na masomo.

"Hatua kali zitachukuliwa kwa mkuu wa shule au mwalimu mkuu yeyote ambaye ataenda kinyume na miongozo iliyotolewa na serikali na walimu walioko kazini na waajiriwa wapya, wafundishe wanafunzi kwa weledi, na bidii ya hali ya juu kwa kuzingatia kalenda ya ufundishaji iliyoko," alisema.

Aliagiza wakuu wa shule, waratibu elimu kata, maofisa elimu wa halmashauri na mikoa yote nchini kufuatilia ufundishaji wa kila siku darasani na kujiridhisha kuwa wanafunzi wanapata umahiri unaotarajiwa kwenye ngazi mbalimbali za elimu ya msingi na sekondari.

"Watumishi wote wa kada za afya nchini, wanaoendelea na utumishi na walioajiriwa wapya, kuhakikisha wanawahudumia wananchi kwa weledi na upendo wa hali ya juu, kwa kuzingatia sheria, kanuni na miongozo ya utoaji bora wa huduma za afya nchini,"

# TAWIRI yaanza uwekaji alama shoroba

**Na Salome Kitomari**

TAASISI ya Utafiti wa Wanyamapori Tanzania (TAWIRI), imesema kazi ya kurejesha shoroba (mapito ya wanyamapori), kwenye hali nzuri inaendelea vizuri, huku ikiomba ushiriki wa wadau wote katika kutunza rasilimali hiyo muhimu.

Mtafiti Mkuu wa TAWIRI, Dk. Steven Nindi, aliyasema hayo wakati wa mkutano wa mtandaoni na waandishi wa habari uliohusu nafasi ya serikali katika kulinda shoroba.

Mkutano huo uliandaliwa na Chama cha Waandishi wa Habari za Mazingira Tanzania (JET), kwa ufadhili wa Mradi wa USAID Tuhifadhi Maliasili.

Dk. Ndindi alisema kuna shoroba 52, kati ya hizo 44 zimepimwa.

Alisema kuna aina mbili za shoroba, mojawapo ni ndefu ambazo zimeunganika kutoka eneo lililohifadhiwa hadi lingine, na aina nyingine ni fupi zenye kuunganisha maeneo ya karibu ili kuwezesha wanyama kupita.

"Duniani kuna shoroba za kutengeneza na za asili, Tanzania tumebarikiwa za asili ambazo zinahitaji kutunzwa kwa kuwa zinawezesha wanyamapori kwenda eneo moja hadi lingine kuzaliana, kupata wachumba, kuoa na kuolewa, kupata madini muhimu ya miili yao," alisema. Dk. Nindi alisema mwaka 1962 Tanzania ilikuwa na tembo 300,000 na hapakuwa na migogoro, sasa wapo zaidi ya 60,000, lakini kumeongezeka migongano kati ya binadamu na wanyamapori hao.

Alisema wanyama kama tembo hawabadilishi njia waliyopita kizazi hata kizazi kutokana na uwezo wao wa kuhifadhi kumbukumbu.

Uwekaji wa alama kwenye shoroba unaendelea, lakini baada ya maelewano na vijiji husika kwa kuwa ndiyo wanaishi pembezoni mwa maeneo hayo wanajua uchungu na utamu wake.

Dk. Joseph Layson wa Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi (NLUPC), alisema kazi kubwa ni kuratibu upangaji ardhi kuanzia taifa, kanda, mkoa, wilaya, kata na kijiji na kwamba wananchi wanashirikishwa katika mpango wa matumizi bora ya ardhi.

Alisema mpango wa matumizi bora ya ardhi uliopo sasa ni wa mwaka 2013 hadi 2033, ukijumuisha mpango wa wilaya 42, vijiji 2,582 na mipango kina ya vijiji 28 kati ya 12,319 vilivyoko nchini.

Dk. Layson alisema: "Lengo la mipango hii ni kuboresha maisha ya watu ili wasiwe na tamaa ya kutumia maeneo yaliyohifadhiwa, kuongeza uzalishaji ngazi ya vijiji na ndiyo maana kuna huduma za umeme."

# Gari la serikali lauzwa mil. 4/- limetembea kilomita 900

**Na Ibrahim Yassin,** SONGWE

MKUU wa Mkoa wa Songwe, Omary Mgumba, amemwagiza Katibu Tawala mkoa huo, Missaile Musa, kumwandikia barua aliyekuwa Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Ileje, mkoani humo kujibu hoja za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), kuuza gari la serikali kwa Shilingi milioni nne.

Mgumba alitoa agizo hilo mwishoni mwa wiki kwenye baraza la kujadili taarifa ya CAG za mwaka 2020/2021 baada ya kuibuka kwa hoja ya gari kununuliwa kwa kiasi hicho cha pesa huku likiwa limetembea kilomita 900 pekee.

Alisema mkurugenzi huyo, Haji Mnasi, alifanya maamuzi ya kuuza gari hilo DFPA yenye namba 8508 aina ya Hilux ambalo halikuwa kwenye orodha ya kuuzwa, na kuuzwa kinyume na utaratibu kwa kutumia nafasi yake ya ukurugenzi.

Pia mkuu huyo wa mkoa alisema, gari hilo mali ya serikali limeuzwa kwa kuiba kadi ya gari kwa mtumishi wa umma ndani ya Wilaya ya Ileje huku akifahamu kuwa ni kosa.

"Katibu Tawala wa Mkoa wasiliana na kamishna ili kupata kadi mpya kwa ajili ya gari hilo ili lirudi kuwa mali ya serikali na kuhakikisha mkurugenzi huyo anarudi kujibu hoja hiyo ili kubaini nini kilimsukuma kuuza gari hilo," alisema Mgumba.

Mkaguzi wa Nje Mkoa wa Songwe, Chausiku Maro, alisema gari hilo lililetwa na kamishna kwa ajili ya matumizi ya mkaguzi wa ndani wa halmashauri hiyo na kuuzwa kumesababisha mkaguzi huyo kushindwa kufika kwa wakati kwenye miradi kwa ajili ya kutekeleza majukumu yake.

"Kama wakaguzi wa nje tumeibua hoja ya kuuzwa kwa gari hilo bila kuwapo kwa nyaraka za vikao halali vya maamuzi na kushauri viongozi wa serikali kuacha kufanya maamuzi kama hayo wakitumia nafasi zao, wanauza mali ya umma kwa masilahi yao wenyewe," alisema Maro.

Mkuu wa Wilaya ya Ileje, Anna Gidarya, alisema watahakikisha wanakuwa bega kwa bega kuhakikisha mali za serikali zinatunzwa na kutumika kwa matumizi yaliyopangwa.

Mwenyekiti wa Halmashauri ya Ileje, Ubatizo Songa, alisema utaratibu uliotumika kuuza gari hiyo bila kibali cha baraza la madiwani, vikao vya wakuu wa idara, vikao vya kamati ya fedha haukuwa sahihi.

Diwani wa Kata ya Ibaba, Tata Kibona alisema gari hilo liliuzwa bila maamuzi ya vikao halali, huku akisema lilikuwa maalumu kwa ajili ya matumizi ya mkaguzi wa ndani.

# PM: Tunaheshimu mchango madhehebu ya dini

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa (pichani), amesema serikali itaendelea kuthamini, kutambua na kuheshimu mchango wa madhehebu ya dini katika kujenga mustakabali wa nchi.

Aliyasema hayo jana katika viwanja vya Ilulu mkoani Lindi wakati wa ibada ya kusimikwa kwa Askofu wa Jimbo Katoliki la Lindi, Wolfgang Pisa.

"Maendeleo ya nchi hayawezi kuimarika kama tutakuwa wabinafsi. Tukiimarisha ushirikiano na ushirikishwaji wa kila mtu, tutaleta maendeleo ya taifa letu kwa haraka," alisema Majaliwa.

Alisema serikali imeendelea kushirikiana na dini zote kukuza ustawi wa wananchi kiuchumi na kijamii ili kuimarisha maisha ya kila Mtanzania na taifa.

Waziri Majaliwa alisema kwa kuzingatia hayo, serikali imekuwa ikishirikiana na sekta binafsi zikiwamo taasisi za dini kutoa huduma mbalimbali kwa wananchi na kuleta maendeleo ya taifa na serikali inatambua na kuthamini kazi na majukumu makubwa ya viongozi wote wa dini.

Majaliwa alisema miongoni mwa majukumu hayo ni pamoja na kuwaongoza watu kiroho kwa kuwapa mafundisho, kutoa



ushauri na kuwajenga kiimani.

"Vilevile, mmekuwa mkiwasaidia watu katika shida mbalimbali husussani wale wenye uhitaji kama yatima na wajane sambamba na kutoa ushauri nasaha na malezi bora kwa vijana," alisema Majaliwa.

Rais wa Baraza la Maaskofu Tanzania (TEC), Askofu Gervas Nyaisonga, akitoa salamu za baraza hilo alisema Kanisa Katoliki limeahidi kuendelea kutoa ushirikiano katika masuala yote ambayo serikali imekusudia kuyafanya kwa ajili ya kuwaletea maendeleo Watanzania.

Nyaisonga ambaye ni Askofu Mkuu wa Jimbo Kuu Katoliki la Mbeya, alisema hivi sasa kanisa hilo linawahamasisha waumini wake kushiriki katika Sensa ya Watu na Makazi itakayofanyika Agosti 23.

Kadhalika, Askofu Nyaisonga aliiomba serikali iendelee kuliunga mkono kanisa hilo katika shughuli mbalimbali linazozifanya katika kuwaletea Watanzania maendeleo ikiwa ni pamoja na suala la elimu na huduma nyingine za kijamii.

Askofu Pisa baada ya kusimikwa aliwashukuru wananchi wa Lindi ambao wamempokea na kuonesha umoja na ushirikiano bila ya kujali madhehebu yao.

Alisema hali hiyo imempa moyo na imani kwamba atafanyakazi kwa kushirikiana na wananchi wote.

Kadhalika, Askofu Pisa alisema kwa sasa jamii imevamiwa na utandawazi ambao umepokelewa na watu wengi na kuleta athari kubwa kiimani, utamaduni na mila, hali inayochangia mmomonyoko wa maadili hususani kwa vijana.

Alisema: "Nawaomba Watanzania wenzangu tubaki katika mila na utamaduni wetu wa asili na tusizolewe na upepo wa utandawazi."


**IN THE COURT OF DISTRICT DELEGATE OF MOROGORO**
**DISTRICT AT MOROGORO**
**PROBATE AND ADMINISTRATION**
**CAUSE NO 70 OF 2022**

In the Matter of the Estate of the Late
**LAZARO GERALD KAHAWA**

**By 1. AGRICOCARS GERALD KAHAWA**
**2. ....................................................**

All persons claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of probate (or letter of administration) is made to the above –named petitioner.
Objection to the grant should be filed on or before the 06 day of 07. 2022
Dated at MOROGORO this 17th day of 06...2022

**RESIDENT MAGISTRATE**



**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**BARAZALA ARDHI NA NYUMBA – MWANZA**
**SHAURI NA 185 LA 2021**
**HAMISA MUSA..........................MUOMBAJI**
**DHIDI YA**

- **SUKARI IZUNGILO MARIBATE**
- **ROMULUS MSUNGA**
- **SUKA SECURITY CO. LTD**
- **ELDANG AUCTIONEERS & GEN BROKER**
- **DANIEL A. LILI**

**WADAIWA**

**KWA: SUKARI IZUNGILO MARIBATE, ROMULUS MSUNGA, SUKA SECURITY CO. LTD, ELDANG AUCTIONEERS & GEN BROKER, NA DANIEL A. LILI**

Mnafahamishwa kwamba Mleta Maombi hapo juu amefungua Shauri / Ombi dhidi yenu katika Baraza la Ardhi na Nyumba Mkoa wa Mwanza. Ombi limepangwa kutajwa tarehe 28/06/2022 katika Chumba cha baraza, Barabara ya Makongoro. Jengo liko mkabala na Mahakama ya Mwanzo Mjini, Tanzania.
Kwa hivyo mnatakiwa kuhudhuria katika Barazasiku hiyo nyie wenyewe, wakili wenu au mtu mwingine anayeruhusiwa kisheria.
KAA- Mkijua kwamba kushindwa kufika, Baraza litasikiliza ombi hilo na kutoa uamuzi bila nyie kuwepo.
Imetolewa name kwa Amri na Chapa ya Baraza leo tarehe 11/05/2022.

**MURIRYA N.**
**MWENYEKITI**
**BARAZALA ARDHI NA NYUMBA**
**MWANZA**



**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**Katika Mahakama ya Mwanzo ya Wilaya ya CHAMWINO MJINI**
**DODOMA MJINI KITUO**
**Mkoa.. DODOMA**
**Usimamizi wa mirathi Na 38/2022**
**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA**
**MAREHEMU ZAINABU SELEMANI MAJENGO WA AREA A**
**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI**
**YALIYOLETWA NA NURU HASSAN BAKARI**

**TANGAZO**
*(Kanuni ya 5(2) ya Kanuni za Usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)*

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu, wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe 14 Mwezi 07 Mwaka 2022 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.
**Zingatia;**
Endapo kuna yeyote mwenye wosia wa Marehemu anaweza kuuleta Mahakamani kukaguliwa.
* Wosia wa marehemu huyo upo mahakamani na waweza kukaguliwa.
* Marehemu hakuacha wosia
* Futa isiyohusika

**Imetolewa leo Tarehe 23 Mwezi 06 Mwaka 2022**


# Wasafirishaji wampongeza Rais Samia

**Na Mwandishi Wetu**

CHAMA cha Wasafirishaji Tanzania (TAT), kimempongeza Rais Samia Suluhu Hassan na serikali kwa kusikiliza na kufanyia kazi maoni yao kwenye Bajeti ya Mwaka 2022/2023.

Taarifa kutoka Ofisi ya Rais wa TAT, Mohammed Abdullah, mwishoni mwa wiki ilisema chama hicho, wanachama na wasafirishaji nchini, wanampongeza Rais Samia kwa kuwasikiliza wasafirishaji wa mizigo.

"Tunayofuraha kubwa kukupa pongezi za dhati kabisa pamoja na wataalamu wako ambao wamekuwa wakifanya kazi nzuri kuishirikisha sekta binafsi katika masuala mbalimbali ya bajeti na kodi.

"Tunashukuru sana kwa punguzo katika kodi ya matrela na vichwa vya magari ya kusafirisha mizigo hadi asilimia sifuri na punguzo katika tozo ya matumizi ya barabara kutoka Dola za Marekani 16 kwa kilomita 100 hadi Dola 10 kwa kilomita 100," alisema katika taarifa hiyo.

Alisema, chama hicho kina imani kuwa changamoto ambazo hazijatatuliwa,

zitafanyiwa marekebisho ili zilete tija katika Sekta ya Usafirishaji na nchi kwa ujumla.

TAT ni chama chenye wanachama wasafirishaji wa mizigo na mafuta zaidi ya 200 nchini. Changamoto katika Sekta ya Usafirishaji zinawagusa moja kwa wanachama wake na wasafirishaji wote nchini.


**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**Katika Mahakama ya Mwanzo Wilaya ya MOROGORO**
**Kituo cha MJINI Mkoa Wa MOROGORO**
**Usimamizi wa Mirathi Na......32 /2021**
**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA**
**MAREHEMU: SHOMARI PANDE WA MJI MPYA-FUMILWA 'B'**

**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI**
**YALIYOLETWA NA: YAHAYA RASHID ULANGA**

**TANGAZO**
**(kanuni ya 5(2)ya Kanuni za Usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)**
Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu,wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tahehe 27 Mwezi 06 Mwaka 2022 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

**Zingatia;**
- Endapo kuna yoyote mwenye wosia na marehemu anaweza kuuleta Mahakamani kukaguliwa.
- Wosia ya narehemu huyo upo mahakamani waweza kukaguliwa.
- Marehemu hakuacha wosia
- Futa isiyohusika.

**Imetolewa Tarehe 20 Mwezi 06 Mwaka 2022**

**HAKIMU**



**THE DISRICT COURT OF MOMBA DISTRICT AT CHAPWA**

CIVIL APPLICATION NO.3 OF 2022
Original Civil Case NO.8 OF 2021
Of the District Court of Momba at Chapwa
ELIZA ADAMSON KILINGO........... APPLICANT
VERSUS
WILES MWENSI LWINGA............. RESPONDENT
TO: WILES MWENSI LWINGA
P.O.BOX 73,
TUNDUMA
TAKE NOTICE THAT: The above mentioned appeal has been fixed foe mention on 28th day of June, 2022 at 08:30 am,and you are required to enter appearance at such time and date.
AND TAKE FURTHER NOTICE THAT, if you default to enter appearance as aforesaid in the appeal, the case will be determined in your absence.
Given under my hand and the seal of the court this 02nd day of June, 2022.

..................................
RESIDENT MAGISTRATE
MOMBA



**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA KILIMO**
**SHIRIKA LA UKAGUZI NA USIMAMIZI WA VYAMA VYA USHIRIKA (COASCO)**

## TANGAZO LA NAFASI ZA KUHAMIA KATIKA SHIRIKA LA COASCO

Shirika la Ukaguzi na Usimamizi wa Vyama vya Ushirika (COASCO) ni Shirika la Umma, lililoanzishwa kwa Sheria Na.15 ya mwaka 1982 kama ilivyofanyiwa marekebisho mwaka 2005. Jukumu Kuu la Shirika ni kufanya ukaguzi wa nje (External Audit) kwa vyama vya ushirika nchini.

Shirika limepewa kibali na Serikali cha nafasi 12 za Watumishi wa Umma kutoka Taasisi zingine za Serikali kuhamia COASCO. Kibali hicho ni kwa watumishi wa umma wa Kada ya Ukaguzi (Audit Officer II) 10 na Kada ya Makatibu Mahsusi (Personal Secretary II) 2.

Hivyo Shirika linawatangazia Watumishi wa Umma ambao wanapenda kuhamia katika COASCO katika nafasi hizo, wenye sifa zifuatazo kwa kila Kada:

**1. Afisa Mkaguzi Daraja la II (Nafasi 10)**

**a) Sifa za Mwombaji**
Wenye shahada ya uhasibu na fedha katika masomo ya ukaguzi na uhasibu (Accounting and Finance) au kuwa na sifa sawa na hizo kutoka katika chuo kinachotambulika na Serikali.

**b) Ngazi ya Mshahara: COASS 4**

**2. Katibu Mahsusi Daraja la II (Nafasi 2)**

**a) Sifa za Mwombaji**
Wenye cheti cha elimu ya Sekondari (CSEE) na kufaulu katika masomo ya Kiingereza na Kiswahili pamoja na kuwa na cheti cha Diploma ya Katibu Mahsusi (Diploma in Secretarial Course) na kufaulu Hati Mkato (Kiingereza) na Hati Mkato (Kiswahili) kwa kasi ya maneno 80 kwa dakika na kuwa na cheti cha weledi wa kompyuta katika (MS-Word, MS-Excel, Internet, Email, MS-Publisher) kutoka katika chuo kinachotambulika na Serikali.

**b) Ngazi ya Mshahara: COASS 2**

**JINSI YA KUOMBA**
Watumishi wa Umma wenye nia ya kuomba hawana budi kuwasilisha barua za maombi zikiambatana na:
i) Taarifa binafsi (CV) zikiwa na majina na anwani pamoja na namba za simu.
ii) Nakala za vyeti vya masomo vilivyothibitishwa (Certified).

**ANGALIZO:**
i) Waombaji lazima wapitishe barua za maombi kwa waajiri wao wa sasa kwani kutofanya hivyo, maombi yao hayatafikiriwa.
ii) Waombaji wote waoneshe nafasi ya kazi wanayoomba juu ya bahasha.
iii) Waombaji watakaokidhi vigezo na kufaulu usaili ndiyo watakaojulishwa kwa hatua zinazofuata.
iv) Waombaji wathibitishe utayari wa kujigharamia uhamisho huo.

Maombi yawasilishwe ndani ya siku kumi na nne (14) tokea tarehe ya tangazo hili kupitia anwani ifuatayo:

Mkurugenzi Mkuu,
Shirika la Ukaguzi na Usimamizi wa Vyama vya Ushirika (COASCO),
S. L. P. 761,
**DODOMA.**

**Au**
**Kwa barua pepe: info@coasco.go.tz**

**Limetolewa leo tarehe**
**27 Juni, 2022**

216920101



Mufti Mkuu, Shekhe Abubakari Zuberi, akizungumza na waandishi wa habari mkoani Dar es Salaam jana, katika uzinduzi wa semina ya mahujaji watakaondoka Julai 3, mwaka huu, kuelekea Maka. Kushoto ni Shekhe wa Mkoa wa Kigoma, Hassan Kiburwa na Meya mstaafu Salimu Londo. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Uazimaji 'mawigi' washamiri, daktari bingwa ataja madhara

**Na Jenifer Gilla**

NI dhamira ya kila mwanamke kuwa na mwonekano mzuri anapokuwa sehemu yoyote yenye watu tofauti iwe ofisini, kwenye biashara au sherehe mbalimbali.

Moja ya kivutio kikubwa cha mwanamke ni kuwa na nywele nzuri, ziwe zimesukwa, kubanwa au kubandika nywele za bandia (wig) ili kuongeza mwonekano mzuri.

Hata hivyo, ili kutimiza haja hiyo kunahitaji kipato cha kutosha kuhakikisha mhitaji anapata vitu muhimu ili mwonekano uwe kama alioudhamiria kwa siku hiyo, watoto wa mjini wanaita "kudamshi".

Wengine hushindwa kumudu gharama za kununua na kutafuta njia rahisi ya kuazima kwenye saluni zinazotoa huduma hiyo.

Baadhi ya saluni zinazopamba wanawake wanaokwenda kwenye sherehe, zimetumia fursa hiyo kukodisha nywele za bandia (mawigi), kwa wanaoshindwa kununua kutokana na kuuzwa kwa gharama kubwa madukani.

Nipashe, ilitembelea baadhi ya saluni za kike zinazotoa huduma hiyo na kuwahoji wafanyakazi na wamiliki wa maduka hayo, akiwamo Mwajabu Salehe, mmiliki wa saluni Tabata, jijini Dar es Salaam, ambaye alisema hufanya biashara ya kuazimisha mawigi ambayo amedumu kwenye kazi hiyo kwa miaka saba na kumsaidia kuongeza kipato chake.

"Huwa ninakodisha kwa siku Sh. 5,000, baada ya saa 24 mtu anatakiwa alirudishe, na siku tatu hadi nne nafanya Sh. 10,000. Kwa wiki naweza kukodisha watu watano hadi 10 kutegemeana na msimu," alisema.

Kwa mujibu wa Mwajabu kwa siku za kawaida anapata faida wastani wa Sh. 70,000 kwa wiki na biashara ikichanganya siku za mwisho wa wiki ambazo watu hutoka kwenye starehe na sherehe mbalimbali hupata Sh. 120,000 hadi Sh. 150,000.

"Kipindi cha kukaribia mwezi wa Ramadhani ndiyo napata wateja wengi wa kuwakodisha kwa sababu ndoa nyingi za Kiislamu hufungwa ambapo kwa siku anaweza kuazimisha mawigi matano na kujipatia Sh. 25,000, lakini msimu wa sikukuu kama Iddi, Krismasi na Mwaka Mpya," alisema.

Naye Hadija Hiza, mfanyabiashara hiyo eneo la Vingunguti, alisema kinachowapa nguvu ya kufanya biashara hiyo ni uhitaji mkubwa wa nywele hizo kadri siku zinavyokwenda kutokana na bidhaa hiyo kuuzwa bei ghali.

"Mawigi wanayoyapenda wengi yanauzwa bei ghali madukani kuanzia Sh. 70,000 hadi 300,000, unakuta wakazi wengi wa Vingunguti uwezo wa kuyanunua hawana, kwa hiyo wakija hapa kwa ajili ya kujipamba tunawakodisha kama hivi, Sh. 5,000 kwa siku mtu akimaliza jambo lake anarudisha," alisema.

**UAMINIFU KWA MTEJA**

Kuhusu uaminifu, Mwajuma alisema mawigi yake hayapotei kwa sababu anaowakodisha ni watu anaowafahamu ni rahisi kuwafuatilia anapoona siku za kurudisha zimezidi na faini ya kuchelewesha ni Sh. 5,000 kwa kila siku itakayozidi.

Theresia Charles (25), mmoja wa wanaokodisha bidhaa hiyo eneo la Vingunguti, anasema huduma ya kukodi mawingi inawasaidia kutimiza haja yao ya kupendeza bila kutumia gharama kubwa.

"Inatusaidia sana sisi wenye kipato cha chini maana laki moja ya kununua wig sina, lakini nikija hapa napata kwa Sh. 5,000 kwa siku kama shughuli ni ya siku tatu au nne nalipia Sh. 10,000 ambayo naitoa mara moja au mbili kwa mwezi," alisema.

**UTUNZAJI**

Ashura Athumani, mmliki wa saluni Tabata Segerea, alisema baada ya wateja kurudishi bidhaa wakishaitumia, huyaosha kwa sabuni ya kuoshea nywele na kukausha kwenye mashine ya kukaushia nywele kabla ya kumpa mteja mwingine.

Hata hivyo, alisema kitendo cha kuyaosha mara kwa mara husababisha kuharibika mapema hali iliyomkatisha tamaa ya kuendelea na biashara hiyo.

"Mimi nilikuwa nakodisha ila sasa nimeacha kwa sababu yamekuwa yakiharibika kutokana na kuyaosha mara kwa mara, wakati mwingine unamkodisha mteja anakwenda kubandika kwenye saluni nyingine anatia gundi nyingi kwa hiyo inabidi utumie nguvu kuitoa nayo inachangia kuharibu," alisema.

**USALAMA KIAFYA**

Daktari Bingwa wa magonjwa ya ngozi kutoka Hospitali ya Lugalo, Dk. Msafiri Kombo, alisema kitendo hicho kina madhara kiafya kwa kuwa kinasababisha magonjwa ya ngozi na kuambukizana ikiwamo mba na fangasi na wadudu kama chawa.

"Hatari ya kuvaa wigi lililovaliwa na mtu mwingine ipo sehemu mbili, hapo mtu anaweza kupata maambukizi ya fangasi au wadudu wanaopenda kukaa kwenye nywele ikiwamo chawa kama litakuwa halijasafishwa na vifaa vinavyoangamiza vimelea vyake," alitahadharisha Dk. Kombo.

Alishauri wanawake wanaopenda urembo huo kuacha kuvaa vitu vilivyovaliwa na watu wengine ikiwamo nguo na mawigi ili kujiepusha na magonjwa ya ngozi yanayoambukizwa.

"Kikubwa wajitahidi wanunue yao wenyewe, kuazimana nguo, viatu na mawigi haishauriwi kiafya, ni muhimu kila mmoja hasa wanawake kuwa makini na vitu kama hivyo kwa sababu wanapoambukizwa wao ni rahisi kuambukiza watu walio ndani ya familia ikiwamo watoto ambao wanakuwa nao kwa ukaribu," alisema.

# Waziri Ummy atoa somo kuepuka kuzaa watoto wenye vichwa vikubwa

**Na Jenifer Gilla**

WAZIRI wa Afya, Ummy Mwalimu, ametoa wito kwa wanawake walio kwenye umri wa kuzaa au wanaopanga kupata watoto, kula vyakula vyenye kuongeza madini ya folic ili kuongeza kinga ya kumkinga mtoto kuzaliwa na mgongo wazi au kichwa kikubwa.

Kwa mujibu wa mtandao wa Office on Women's Health (OASH), wa Idara ya Afya na Huduma za Binadamu nchini Marekani, Folic Acid ni madini yanayotokana na mboga, matunda na mazao jamii ya karanga vyenye vitamin B9 ikiwamo mahindi, maharagwe, choroko, spinachi, papai na parachichi yanayosaidia kujenga ubongo wa mtoto na uti wa mgongo katika wiki tatu za mwanzo tangu mimba kutungwa.

Waziri Ummy aliyasema hayo jana baada ya kushiriki mbio za marathon, zilizoandaliwa na Taasisi ya Mifupa (MOI), kwa ajili ya kuchangisha fedha za matibabu kwa watoto 200 wenye tatizo la kichwa kikubwa.

Alisema tatizo hilo linatokana na ukosefu wa madini ya Folic Acid, na linaweza kuzuilika ikiwa wanawake waliotayari kuzaa wakitumia dawa hizo.

"Watoto wanaozaliwa na changamoto ya kichwa kikubwa na mgongo wazi bado ni tatizo hapa nchini. Takwimu zinaonyesha katika nchi tano barani Afrika zenye watoto wanaozaliwa na mgongo wazi na kichwa kikubwa Tanzania tupo namba tatu tukitanguliwa na Algeria na Ethiopia," alisema.

Waziri Ummy alisema, katika kila watoto 1,000 wanaozaliwa kwa mwaka, watatu huzaliwa na tatizo hilo.

Alisema ili kuzuia watoto wenye tatizo hilo nchini, serikali inaendelea kuboresha huduma ya uzazi hususani kabla ya kujifungua, wakati wa ujauzito na wakati wa kujifungua.

Ili kutimiza azma hiyo, Waziri Ummy aliwaagiza waganga wakuu wa mikoa na wilaya kuhakikisha madini hayo yanapatikana kwa urahisi katika ngazi zote za kutolea huduma ya afya hadi zahanati.

Alitoa wito kwa wazazi na walezi kutowaficha watoto wanaozaliwa na matatizo hayo kwa kuwapeleka kwenye vituo vya kutolea huduma ya afya ili wafanyiwe upasuaji.

# Mamlaka dawa za kulevya kuongezewa makali

**Na Salome Kitomari,** DODOMA

SERIKALI imewasilisha bungeni muswada wa mabadiliko na kuondoa baadhi ya vifungu vya sheria mbalimbali.

Sheria hizo ni ya Kuzuia Usafirishaji Haramu wa Binadamu, Sura ya 432, Sheria ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya, Sura ya 95 na Sheria ya Kanuni za Maadili ya Viongozi wa Umma, Sura 398.

Muswada huo wa mabadiliko ulisomwa kwa mara ya kwanza mwishoni mwa wiki bungeni, na ulisainiwa na Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Jaji Eliezer Feleshi.

Sehemu ya tatu ya muswada huo unakusudia kufanya marekebisho katika Sheria ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya, sura ya 95 kwa kifungu cha pili kinafanyiwa marekebisho, ili kujumuisha kemikali bashirifu au mchanganyiko wake katika orodha ya dawa zilizokatazwa.

"Madhumuni ya marekebisho haya ni kudhibiti dawa ambazo matumizi yake yanaweza kuchepushwa na hatimaye kutengeneza dawa za kulevya ambazo zimekatazwa na sheria hii," alisema.

Mengine ni kufuta na kuandika upya kifungu cha 32, kwa ajili ya kutoa madaraka kwa maofisa wa mamlaka, ili wawe na nguvu za kisheria sawa na mamlaka ya maafisa wa polisi chini ya Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai au mamlaka ya maofisa forodha chini ya Sheria ya Forodha.

Vile vile, sharti linaongezwa kwa ofisa wa mamlaka ya kupambana na dawa za kulevya kuwasiliana na kushirikiana na mamlaka nyingine kutakapokuwapo na uhitaji.

"Madhumini ya marekebisho haya ni kutoa nguvu za kutosha kwa maofisa wa mamlaka wakati wa utekelezaji wa majukumu yao," alisema.

Pia sheria inarekebishwa kwa kuongeza kifungu cha 32A kwa kutoa mamlaka kwa Mkurugenzi Mkuu au ofisa mwidhiniwa wa mamlaka kuwa na uwezo wa kutoa hati za upekuzi.

"Madhumuni ya marekebisho haya ni kutoa nguvu kwa mamlaka katika shughuli za upelelezi hasa pale mamlaka inapotakiwa kuchukua hatua za haraka ili kuzuia kuharibu ushahidi," alisema.

Aidha, mamlaka imepewa ridhaa ya kuanzisha maeneo ya kuwaweka watuhumiwa kabla ya kufikishwa mahakamani, kwa dhumuni la kuweka mazingira wezeshi kwa mamlaka kutekeleza majukumu yake.

Pia sehemu ya nne ya sheria inapendekezwa kufanyiwa marekebisho kwa kufuta kichwa cha habari kinachosomeka 'taratibu za ukamataji' na badala yake kuandika 'taratibu kuhusiana na upelelezi'.

"Madhumuni ya marekekisho haya ni kuandika kichwa cha habari ambacho kinaakisi ujumla wa masuala yote yanayotekelezwa na mamlaka chini ya sehemu hii. Pia yanapendekezwa kufanyiwa katika kifungu cha 48 kwa lengo la kuipa Sheria ya Kupambana na Dawa ya Kulevya nguvu dhidi ya sheria nyingine yoyote inayokinzana nayo.

USAFIRISHAJI BINADAMU

Muswada huo unapendekeza marekebisho ya Sheria ya Kuzuia Usafirishaji Haramu wa Binadamu Sura ya 432 kwa kurekebisha vifungu vya 4, 5, 6, 7, 8A na 13 kwa ajili ya kuongeza adhabu zilizoainishwa katika vifungu tajwa, kwa lengo la kuongeza adhabu na kupunguza utendaji wa makosa.

Pia sehemu ya nne ya muswada inapendekeza kurekebisha Sheria ya Kanuni za Maadili ya Viongozi wa Umma, Sura ya 398, kifungu cha tisa kinarekebishwa ili kuweka ukomo wa muda ambao mtu anapaswa kuwasilisha tamko la mali na madeni wakati anapoacha kuwa kiongozi wa umma.

"Marekebisho yanayopendekezwa yanalenga kuboresha usimamizi wa utekelezaji wa masharti ya kifungu cha tisa ya kiongozi kutoa tamko la mwisho.

"Kifungu cha 10 kinachohusu mali zisizopaswa kutamkwa kinapendekezwa kufutwa na kifungu cha 11 kinapendekezwa kurekebishwa kwa kuongeza aya mpya katika orodha ya mali zinazopaswa kutamkwa. Marekebisho yanayopendekezwa yana lengo la kuondoa mkanganyiko katika utekelezaji wa sheria kwa kuwa na kifungu kimoja tu kinachoainisha mali zinazopaswa kutamkwa pekee."

Mengine ni kurekebisha kifungu cha 19 kwa kuongeza baada ya aya (e), zinazoongeza majukumu ya sekretariati kwa madhumuni ya kuelekeza wajibu wa sekretariati katika kuhamasisha maadili.

# Atupwa jela miaka 30 kwa kubaka

**Na Joctan Ngelly,** GEITA

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Mkoa wa Geita, imemhukumu mkazi wa Mbugani, Sefu Almas (19), kutumikia kifungo cha miaka 30 jela kwa kosa la kubaka msichana mwenye umri wa miaka 14 na kumsababishia maumivu.

Mshtakiwa huyo alipandishwa kizimbani mbele ya Hakimu Mkazi Mfawidhi wa Mahakama hiyo, Cleofas Waane na aliposomewa shtaka lake alikiri kumbaka msichana huyo akidai kuwa alikuwa mpenzi wake. Hakimu Waane alisema kwa kuwa mshtakiwa amekiri kosa lake bila ya kulazimishwa, mahakama inamtia hatiani kwa kosa aliloshtakiwa.

Alipotakiwa kujitetea, mshtakiwa alidai kuwa msichana huyo alikuwa mpenzi wake na kuiomba mahakama imwachie huru.

Hakimu Waane alitupilia mbali utetezi huo na kusema kitendo alichokifanya ni cha kikatili na mahakama hiyo inamhukumu kwenda jela miaka 30 ili akajifunze namna ya kuishi na jamii.

Upande wa mashtaka ukiongozwa na Wakili wa Serikali, Monika Matwe, uliiomba mahakama itowe adhabu kwa mujibu wa sheria.

Akisoma hati ya mashtaka Wakili wa Serikali, Matwe alidai, kati ya Machi hadi Mei mwaka huu, katika eneo la Nyankumbu, Mkoa wa Geita, mshtakiwa alimbaka msichana mwenye umri wa miaka 14 na kumsababishia maumivu makali sehemu zake za siri kitendo ambacho ni kinyume cha sheria.


# CONSULTANCY ADVERT

**Location** : Monduli - Arusha
**Application Deadline** : 05 July 2022
**Languages Required** : English and Swahili

**(Date when the selected candidate is expected to start) 8th July 2022**

Ujamaa-Community Resource Team (UCRT) is a non-profit environmental and social justice organization, which works with indigenous groups of different cultures. The target communities are those who depend on communal resource management regimes to support their livelihood.

**1. CONSULTANCY SERVICE FOR UNDERTAKING BASELINE SURVEY**

Objective. Undertake a comprehensive baseline study to understand the current and historical environmental, economic, social, and political factors that may enable or hinder connectivity and effective, equitable and sustainable natural resource governance in Kwakuchinja. The study will consider, but not be limited to, the six villages, including exploring the state of land and natural resource governance in them. Key data gaps will be noted, with plans for how critical gaps can be addressed within the project.

**Specific tasks and scope of the consultancy service**
- Assessing the current situation of cooperatives in Kwakuchinja in terms of historical development, existing obstacles and challenges.
- Propose and discuss report structure and format with the planning team (content presentation, best use of case studies, visual elements, Use of graphs and charts etc.)
- Submitting and presenting the final report to the organization.
- Finalizing the final draft report with comments been incorporated
- Submit one soft and hard copy of the final report to the organization

**Qualifications and Experience**
- Consultant(s) must have Advanced University Degree (Masters or equivalent) in Gender Studies, Social Sciences, Human Rights, Development Studies, or related field.
- At least five (5) years of relevant professional experience in designing and delivering land and natural resources in the Public Sector, International or Regional Organization.
- Demonstrated experience in advocating gender and land rights.
- Proven experience in report writing demonstrated through at least 2 samples
- Fluency in spoken and written English and Swahili. Knowledge of MAA will be an added advantage.

**2. CONSULTANCY SERVICE FOR LIVESTOCK COOPERATIVE DEVELOPMENT**

**Objective;** Support the establishment, capacity building and quarterly assessment and monitoring of the existing cooperatives and encourage livestock keepers, particularly youth and women, to buy and sell livestock to increase livestock productivity and poverty reduction.

**Specific tasks and scope of the consultancy.**
- Mapping the existing women cooperatives in kwakuchinja and collaborate with UCRT to set criterial for establishing livestock cooperatives.
- Providing support in terms of trainings to the existing cooperatives for capacity building and pay quarterly visit of the group.
- Develop business plan with cooperative members.
- Providing support, technical knowledge and a road map for setting up women cooperatives (start-ups) to relevant stakeholders.
- Submitting and presenting the final report to the organization.
- Finalizing the final draft report with comments been incorporated

**Qualifications and Experience**
- Consultant(s) must have Advanced University Degree (Masters or equivalent) in Economic studies, Development Studies, or related field.
- At least five (5) years of relevant experience in cooperative development.
- Demonstrated experience in advocating gender and land rights.
- Proven experience in report writing demonstrated through at least 2 samples
- Fluency in spoken and written English and Swahili. Knowledge of MAA will be an added advantage.

**Applications documents**
- Application letter
- Technical and financial proposal
- Business registration/certificate of incorporation
- TIN Certificate
- Business license
- Evidence for use of EFD machine

**Duration of the consultancy:**
The task will take a total of three weeks from **05st to 30th July 2022**

**Submission**
The interested company, firms, or individuals are requested to submit their application in electronic copy to **manager@ujamaa-crt.or.tz** not later than **05 July 2022.**

ADDRESS

**EXECUTIVE DIRECTOR**
**UJAMAA COMMUNITY RESOURCE TEAM**
**P.O. BOX 15111**
**ARUSHA-TANZANIA**

216919701

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Tuzilinde sanaa zetu zisipoteze uasili wake

**KATIKA** karne ya 21 teknolojia ya televisheni na maonyesho mbalimbali vimeitangaza sanaa ya tasnia ya filamu kwa watu wote; watazamaji wa mijini na vijijini katika nchi nyingi zinazoendelea.

Hata hivyo, filamu nyingi zinazosambazwa kimataifa na kupenya soko la nchi nyingi ni zile zinazozalishwa Marekani na baadhi ya nchi za Ulaya.

Filamu pia zimekuwa zikitumika kama njia muhimu ya uchumi, hali iliyofanya kuwa nyenzo muhimu itumiwayo na nchi za Ulaya na Amerika.

Mwanzoni mwa miaka ya 1970, dunia ilishuhudia utengenezwaji wa sinema zipatazo 3,500 kila mwaka. Ingawa ni asilimia tano tu ya sinema hizi zilitengenezwa Marekani, lakini filamu za Marekani ndizo zilizochukua asilimia 50 ya muda katika vituo mbalimbali vya televisheni.

Mafanikio ya masoko ya filamu na televisheni ya Marekani kwa kiasi kikubwa yametokana na mkusanyiko wa kampuni za Marekani, Vyama vya Wasanii na kampuni kubwa ambazo zimewekeza fedha nyingi.

Kusambaa kwa wingi kwa filamu za Magharibi katika nchi zinazoendelea inachukuliwa kama hali ya kutiliwa wasiwasi na makundi mengi, kwamba filamu hizo zinaweza kubadilisha hali ya kisiasa na kiuchumi ya nchi zinazoendelea na hata mitazamo ya maisha.

Kama mipango madhubuti haitaweza kufikiwa na serikali zetu, hofu za wengi kuhusu ukandamizaji wa kisiasa zitaongezeka.

Filamu huweza kutoa ujumbe tofauti kwa kila mtazamaji na huweza kushawishi na kutoa taswira ya kipekee kwa kila mtu binafsi, hivyo, tunapaswa kuwa makini na kupima matokeo ya athari zinazosababishwa na filamu zinazoweza kupatikana ama kwa mtu binafsi au watazamaji wote.

Mtazamo wa filamu za Magharibi, hasa Hollywood kuhusu nchi zinazoendelea ni wa kisiasa kabisa. Filamu hizo hutengenezwa kwa malengo maalumu na huweza kuacha athari miongoni mwa watazamaji.

Tafiti zilizofanywa zimeonyesha kuwapo ushawishi mkubwa wa filamu katika majukumu ya kijamii na mahusiano katika nchi zinazoendelea.

Baadhi ya wachambuzi wanasema kwamba kama utamaduni wa asili utaridhia mahitaji ya watu, ni jamii ndogo tu ya watu itakayobaki imara kwenye maadili yanayotishiwa na vyombo vya habari vya kigeni.

Tafiti zingine kuhusu kubadilishana tamaduni zimegundua kwamba yatokanayo na vyombo vya habari vya Magharibi yanaongezeka katika kuleta athari kwa mtu mmoja mmoja, ingawa yana faida pia kama elimu na kuongezeka kwa uwezo wa uelewa.

Wakati vijiji na miji katika nchi zinazoendelea ikizidi kuwa na mtandao mpana wa upatikanaji wa filamu za Magharibi na video, nchi nyingi za Magharibi wana nafasi finyu sana ya kuona hali halisi ilivyo katika vijiji na miji ya nchi zinazoendelea ili kuwezesha kuwa na uelewa unaofanana.

Filamu za nje zinazopatikana Marekani nyingi hutengenezwa katika nchi za Ulaya, mara nyingi kwa ufadhili wa Marekani yenyewe.

Wachambuzi wengi wa nchi zinazoendelea wanahofu kwamba nchi zetu sasa zijiandae kupoteza kilicho chao na kupokea mambo na tamaduni za kigeni na kuwa katika hatari ya kuendeleza mazao ya Magharibi badala ya tamaduni zetu.

Utamaduni wa nchi ni "kidhibiti mwendo" kinachoongoza mwenendo na tabia za watu katika jamii, ni msingi wa maisha ya mtu binafsi kumwezesha kujitambua, kuwa na mwelekeo na kujichagulia falsafa sahihi ya maisha yake.

Nchi zinapaswa kuanzisha sera muhimu za kulinda haya ili kudhibiti umilikaji wa wageni wa kuagiza vitu toka nje, kupiga marufuku filamu zinazoingizwa kiholela, ukaguzi wa mara kwa mara, udhibiti wa maudhui ya filamu na tamthilia, na kutoa ruzuku kwa watengenezaji filamu wa ndani.

Kufuatia sera hizi umma uelimishwe kikamilifu juu ya sera hizi ili uweze kushiriki katika utekelezaji kwa upana wake. Pia ushirikishwaji wa vyombo vya habari katika kusaidia msukumo wa wananchi kuielewa sera ya utamaduni upewe nafasi ya kutosha.

Jambo muhimu na la msingi ni kuzingatia, kuzitambua na kuzilinda sanaa zetu ili zisipoteze uasili wake pamoja na wimbi la mabadiliko ya wakati na mazingira ya sasa ya utandawazi na biashara huria.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Adam Fungamwango

# Kalolanya anavyotuambia benchi si adui

**UKIMWONA** kwa sasa akiwa golini na jinsi anavyofanya kazi yake kwa ustadi unaweza ukadhani kwamba Simba na ina golikipa mpya.

Kwa mechi kadhaa sasa ambazo Simba imeonekana kuukosa ubingwa wa Tanzania Bara kuna golikipa mwingine ambaye anakaa golini.

Anadaka michomo kwa ustadi na 'saves' za maana kiasi cha kuwakosha mashabiki wengi waliopo uwanjani na wale ambao wanamtazama kwenye televisheni.

Kuna watu wameshaanza kusema kuwa alikuwa wapi huyu, si bora angekaa hata mechi zingine za huko nyuma?

Huyu ni Beno Kakolanya. Kipa namba mbili wa Simba ambaye wanachama na mashabiki wengi wa timu hiyo walikuwa hawamwamini. Asipokuwapo Aishi Manula roho zao zikakaa juu kama mkungu wa ndizi.

Hii ilisababisha msimu huu kumsajili Jeremiah Kisubi, ambaye dirisha dogo akapelekwa Mtibwa Sugar kwa mkopo.

Wengi wanashangaa kiwango hiki anachoonyesha sasa Beno amekipata wapi wakati kila msimu yeye ni mtu wa benchi?

Kiwango chake cha sasa kimesababisha mashabiki wa Simba kudai kuwa hata kwenye mechi za Ligi Kuu au Ligi ya Mabingwa kama Manula akiumia hawana wasiwasi tena, wanajua wana mtu golini.

Kwa siku za karibuni tangu mechi ya fainali ya Kombe la FA, Kakolanya amefanya kazi kubwa ambayo si mashabiki wa Simba tu, bali hata wa soka kwa ujumla wamemkubali.

Na sidhani kwa misimu ya hivi karibuni inaweza kwenda sokoni kutafuta makipa, badala yake itakuwa inalea makipa vijana ambao watakuja kuwa namba tatu.

Mashabiki wengi wa soka wanadhani kuwa mchezaji kucheza mechi nyingi ndiyo dawa ya kulinda kipaji chake, na kama hapati muda mrefu wa kucheza, kipaji kinadumaa au kushuka.

Hiyo tumeona mara nyingi wachezaji ambao wanakaa benchi hasa wa Kitanzania, viwango navyo vinakuwa hivyo hivyo kwa kibenchi.

Hapa Bongo utaona kabisa hata uwanjani tofauti na mchezaji wa kikosi cha kwanza na yule anayetokea benchi.

Inaonekana ni kama anayeingia anakwenda kutimiza idadi ya wachezaji 11 kwa sababu yule tegemeo amechoka, au hayuko vizuri siku hiyo.

Kakolanya hakupata nafasi sana ya kucheza ni kutokana na uwepo wa Manula, ambaye amekuwa mlinda mlango namba moja wa Simba hakuna asiyefahamu uwezo wa Manula.

Pamoja na kwamba amekaa kwa muda mrefu benchi, lakini nafasi chache alizopata za kucheza, anachokifanya ni kinyume na matarajio ya watu wengi, Wengi walitegemea kumuona Beno akifanya makosa ya mara kwa mara kwa sababu ya kutokaa golini kwa kipindi kirefu, si kwenye Ligi ya Mabingwa, Shirikisho, Ligi Kuu au FA Cup.

Beno anatoa somo kubwa sana anatuambia kwa vitendo kwamba unapopatiwa nafasi fanya watu wasiwaze kuhusu yule uliyechukua nafasi yake, badala yake wafikirie kuhusu wewe.

Mechi zote alizocheza amesimama golini vyema, tena kwa kujaribiwa na tumeona 'saves' zake za maana pamoja 'clean sheets. Kifupi watoto wa mjini wanasema, amefanya kweli.

Inaonyesha kabisa kuwa pamoja na kwamba Manula alikuwa anacheza mechi nyingi, lakini Kakolanya hakukata tamaa, au kuwa na kinyongo, au kulazimisha kuondoka ili akapate nafasi ya kucheza kwenye timu zingine, badala yake alikomaa na kupigania namba.

Japo bado ukweli ni kwamba Manula ataendea kuwa namba moja, lakini naye itaanza kumfikirisha na kujituma zaidi, kwani uzembe wowote ule au kutokuwa makini, kunaweza kumfanya kukaa benchi na Kakolanya kuchukua nafasi yake.

Bahati nzuri ni kwamba tayari mashabiki wameshamuona jinsi alivyopandisha kiwango chake, hivyo hakuna yoyote atakayepiga kelele.

Hili liwe somo sasa kwa wachezaji wengine kuwa kukaa benchi siyo kama hujui, au kukufanya ubweteke, usijitume mazoezini, la hasha.

Unatakiwe upambanie namba, siyo kujihisi mnyonge na kutaka kuondoka ili kupata sehemu rahisi ya kwenda kucheza. Namba siku zote haina mwenyewe, atakayecheza vema ndiye atakayecheza.

Mchezaji yoyote anayetokea benchini atakiwa kufanya sana mazoezi na kujua udhaifu yake unaosababisha kutokuwepo kikosi cha kwanza, akaufayia kazi.

Inatakiwa dakika chache zile zile hata kama ni tano utakazopewa, unatakiwa kuzifanyia kazi ili si kocha wala benchi la ufundi tu, bali hata mashabiki wajiulize ni kwa nini unakaa nje.

# Waadhimisha Siku Uchangiaji Damu chupa 33

**Na Mary Kadoke**

WAFANYAKAZI wa Benki ya DTB wamechangia damu chupa 33 kwa Mpango wa Taifa wa Damu Salama (NBTS), ikiwa ni mkakati wa kuadhimisha Siku ya Uchangiaji Damu Duniani.

Akizungumza na Nipashe, Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano na Masoko wa DTB, Sylvester Bahati, alisema tukio hilo lililofanyika mwishoni mwa wiki jijini Dar es Salaam, kuadhimisha siku hiyo.

"Tukio hili limelenga zaidi kuchangia damu na kama DTB huwa na mwenendo wa kujitolea kama wafanyakazi kurudisha kwa jamii na miongoni mwa shughuli hizo kuchangia damu chupa 33," alisema Bahati.

Alisema jamii haina budi kuelewa umuhimu wa uchangiaji damu kwa kuwa ndiyo wanaotarajiwa kutatua upungufu wa damu kwa watu wenye uhitaji hospitalini.

"Benki ya damu salama wanakuambia sisi tunaochangia hatukidhi hata asilimia 30, kwa hiyo kama jamii ni jukumu letu kuchangia upungufu uliopo katika benki hiyo ili kuokoa maisha," alisema.

Ofisa Ustawi wa Jamii wa NBTS, Kanda ya Mashariki, Mariamu Juma, aliwashukuru wafanyakazi wa DTB kujitolea damu kwa watu wenye uhitaji hospitalini.

"Tupo na Benki ya DTB, kwamba wafanyakazi pamoja na watu wa karibu na maeneo haya wanachangia damu. Kama kitengo cha damu salama tunaishukuru DTB kwa kuunga mkono juhudi za serikali katika kupambana na wagonjwa wenye upungufu wa damu katika hospitali zetu," alisema na kuongeza:

"Tunawashukuru kwasababu damu hii inaenda kuokoa makundi mbalimbali yenye uhitaji wa damu kama kinamama wanaojifungua, wagonjwa wa ajali, watoto na wanaofanyiwa upasuaji wa moyo na wagonjwa wengine wenye uhitaji wa damu."

Alisema dhima ya Benki ya DTB iko katika maeneo matatu, afya elimu na mazingira, hivi karibuni walifanya usafi katika ufukwe wa Coco wakati wa maadhimisho ya Siku ya Bahari Duniani.



Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga, Sophia Mjema, akizungumza kwenye kikao Maalum cha Baraza la Madiwani Manispaa ya Shinyanga kujadili taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi wa Hesabu za Serikali (CAG) kwa mwaka wa fedha 2020/2021 jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Jukwaa 'GO na NMB' lazinduliwa Zanzibar

**Na Mwandishi Wetu**

BENKI ya NMB imezindua rasmi jukwaa la kuwawezesha vijana visiwani Zanzibar kuwasaidia kujenga kiuchumi na kuwakwamua kifedha kwa kuwahudumia kidigitali, kuwakopesha na kuwapa elimu ya fedha maarufu kama 'GO na NMB'.

Ofisa Mtendaji Mkuu wa NMB, Ruth Zaipuna, alisema benki hiyo imejipanga kikamilifu kuwafanya vijana wa Zanzibar kuwa na nidhamu ya kutumia pesa ili wawe raia wanaowajibika vyema kifedha.

Aliyasema hayo juzi, wakati wa uzinduzi rasmi wa jukwaa hilo uliofanyika Forodhani, mgeni rasmi akiwa Makamu wa Pili wa Rais, Hemed Suleiman Abdulla.

Abdulla alisema uwekezaji huo ni chachu hitajika ya maendeleo na kuwa jukwaa hilo ni maalum kwa vijana na mwendelezo wa mkakati wa benki hiyo kuboresha huduma zake na kuongeza mchango wa kisekta kwa makundi mbalimbali ili kusaidia juhudi za serikali za kukuza uchumi.

"Jukwaa tunalozindua leo linatoa suluhu kwa changamoto mbalimbali zinazoikabili sekta ya fedha. Linakuja na fursa nyingi hasa kwa vijana kama mikopo, rasilimali fedha na bidhaa nyingine kama MastaBoda, Mastaboti na pia kutoa elimu ya kifedha," alisema Zaipuna.

Vile vile, alisema kuwapa vijana elimu ya fedha ni suala la msingi kutokana na wingi wao ambao sasa hivi ni asilimia 64 za watu wote nchini.

Alitaja fursa nyingine zinazopatikana katika jukwaa hilo kuwa ni pamoja na mikopo ya vitendea kazi (Mastaboda), Mastaboat, kufahamu matumizi na faida za huduma za kidigitali, NMB Lipa Mkononi, MshikoFasta na NMB Pesa Wakala.

Fursa nyingine ni mafunzo ya programu za huduma jumuishi za kifedha, bima ya bure ya simu za mkononi na kupata fursa za ajira kupitia mafunzo ya usimamizi. Fursa za kuhudhuria matukio mbalimbali kama makongamano ya wanafunzi vyuoni na mafunzo ya ujasiriamali.

Makamu huyo alisema jukwaa hilo ni jambo jema linaloendana na juhudi za serikali za kutatua changamoto zinazowakabili vijana na kuwashirikisha katika ujenzi wa taifa.

Alisema jukwaa hilo ni uwekezaji wenye tija kwa sababu ya kuwainua vijana kifedha na kiuchumi kutakakosaidia kukabiliana na tatizo la ukosefu wa ajira na kuwasihi kuzingatia elimu ya masuala ya kifedha ambayo iko chini ya asilimia 30 na upatikanaji wa mitaji kirahisi.

"Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inatambua na kutoa kipaumbele katika kuendeleza vijana kwa dhamira ya kujenga uwezo wa kujitegemea kuliko kutegemea ajira kama chanzo cha mapato yao. Kwa kuzindua mpango huu leo, vijana wataanza kutambua umuhimu wa kujiwekea akiba na pia kutumia teknolojia kujipatia faida mbalimbali," alisema.

Mkuu wa Wilaya ya Zanzibar Mjini, Rashid Simai Msaraka, alisema jukwaa la GO na NMB limezinduliwa kwa wakati muafaka kwa kuwa wakazi wengi wa visiwa hivyo kwa muda mrefu wanakabiliwa na tatizo la kukopa fedha kwa riba kubwa.

Jukwaa hilo kwa mara ya kwanza lilizinduliwa jijini Dar es Salaam mwaka jana na Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge, Kazi, Vijana, Ajira na Watu Wenye Ulemavu), Patrobas Katambi.

## Mtendaji Kijiji atuhumiwa upotevu mil. 3.4/-

**Na Sabato Kasika**

OFISA Mtendaji wa Serikali ya Kijiji cha Juhudu B, wilayani Ruangwa, mkoani Lindi, anatuhumiwa kupoteza zaidi ya Sh. milioni 3.4 za wananchi wa vijiji vya Juhudi A na B.

Fedha hizo ni sehemu ya zaidi ya Sh. milioni 8.2 zilizokusanywa na Kamati ya TASAF kutoka kwa wananchi maskini wa vijiji sita vya Kata ya Chingongwe, ikiwa ni michango yao ya kusajiliwa katika huduma ya matibabu kupitia mpango wa Mfuko wa Afya Jamii vijijini (CHF).

Tuhuma hizo zimeibuliwa kwenye semina ya mafunzo ya utawala bora yanayoratibiwa na Jukwaa la Elimu ya Uraia Tanzania 'Civil Education Forum in Tanzania' (CETA), inayoshirikisha wenyeviti na watendaji wa vijiji, watendaji wa kata, madiwani na wenyeviti wa kamati kudumu za jamii.

Mradi huo uliozinduliwa na Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, Aprili 14, mwaka huu, umefadhiliwa na Shirika la Kimataifa la Ujerumani la Hanns Seidel Foundation (HSF), ambalo ofisi zake zipo jijini Dar es Salaam.

Aliyeibua tuhuma hizo ni Mwenyekiti wa Kijiji cha Juhudi B, Jafari Lwidi, ambaye alimtuhumu Ofisa Mtendaji huyo Mohamed Makota, kutafuna kiasi hicho cha fedha na kusababisha malalamiko kwa wananchi.

Mtuhumiwa alikiri kupokea fedha hizo Sh. milioni 3.4, na kufafanua kuwa hajatumia vibaya, bali watu wasiojulikana walivamia nyumba yake usiku na kuiba fedha, redio na televisheni wakati akiwa nje ya kijiji kwa matibabu.

"Tayari nimeanza kurejesha fedha hizo kwa kutoa Sh. 930,000, ninatarajia kukamilisha malipo ya deni hilo ifikapo mwishoni mwa Agosti, mwaka huu, hivyo tuvumiliane," alifafanua Makota.

Ofisa Maendeleo ya Jamii wa Kata ya Chinongwe, Novath Kweka, alithibitisha kuwa Kamati ya TASAF, ilimkabidhi fedha hizo Makota na kumwelekeza kuzipeleka benki kama miongozo inavyotaka.

"Suala hilo ni kweli limetokea, ndiyo maana wakati Mkuu wa Wilaya ya Ruangwa, Hassan Ngoma, alipotembelea Kata ya Chinongwe Juni 14, mwaka huu, alijulishwa na kuagiza polisi kumkamata Makota," alisema Kweka.

Ofisa Utumishi wa Wilaya ya Ruangwa, Julius Mukheben, amethibitisha tukio hilo na kwamba mtuhumiwa aliwahi kukamatwa na Jeshi la Polisi kisha kuachiwa na ameanza kulipa fedha hizo.

Mukheben alifafanua kuwa kwa sasa wanasubiri mtumishi huyo amalize kulipa fedha zote ndipo hatua mojawapo kati ya hizo mbili ichukuliwe, kumfukuza kazi au kumshusha cheo.

# Aliyefungwa kwa kumtukana mama mzazi aachiwa huru

**Na Grace Gurisha**

MAHAKAMA Kuu Kanda ya Dar es Salaam, imetengua hukumu iliyotolewa na Mahakama ya Wilaya ya Ilala dhidi mfanyabiashara, Zarina Mohamed Sidik, aliyehukumiwa kifungo cha mwaka mmoja jela kwa kosa la kumtukana mama yake mzazi.

Uamuzi huo ulitolewa na Jaji Juliana Masabo wa mahakama hiyo.

Alisema mrufani (Zarina) alikuwa na hoja saba za kupinga hukumu hiyo iliyomtia hatiani ikiwa ya Mahakama ya Ilala kukosea kumtia hatiani na kumfunga mrufani kwa kuwa mashtaka dhidi yake hayakuthibitishwa pasipo kuacha shaka na upande wa mashtaka.

Alisema mahakama hiyo pia ilikosea kumtia hatiani Zarina na kumfunga kwa sababu kulikuwa hakuna ushahidi uliotolewa dhidi yake na mahakama hiyo haikuchambua ipasavyo ushahidi, kwa kuwa ushahidi wa upande wa mashtaka haukuwa na uhakika.

Pia Jaji Masabo alisema ushahidi wa mrufani haukuzingatiwa na ushahidi wa mashtaka ulikuwa wa kusikia na sio wa kuungana jumuishi.

Jaji Masabo alisema mrufani alidai kuwa mashtaka dhidi yake hayajulikani, kwamba alitoa lugha ya matusi dhidi ya mama yake Novemba 29, 2019 haikufafanua muda gani alitoa lugha hiyo.

"Ingawa inadaiwa kuwa mrufani alito lugha hiyo ya matusi mbele ya mteja wake, lakini mteja wake hakuja kutoa ushahidi mahakamani," alisema Jaji Masabo na kuongeza:

"Kutokuitwa kwa shahidi huyo ambaye alikuwa ni shahidi wa muhimu katika kesi hiyo, kunafanya mashtaka dhidi mrufani kutothibitika."

Jaji Masabo alisema wakati Wakili wa Zarina anatoa hoja zake, alieleza kuwa mahakama haikutambua kama maneno yaliyozungumzwa yalikuwa ni matusi au la.

Aliendelea kufafanua kuwa dukani hapo kulikuwa na CCTV kamera, ilitarajiwa upande wa mashtaka ungewasilisha ushahidi huo, lakini haukufanyika hivyo.

Jaji Masabo alisema: "Mahakama baada ya kusikiliza hoja pande zote mbili, nakukubaliana na wakili wa mrufani kwamba kesi dhidi yake haijathibitishwa, hivyo hatia na kifungo dhidi ya mshtakiwa imeondolewa na ameamriwa ya kwamba aachiwe labda kama anashtakiwa na kesi nyingine kisheria."

Hukumu hiyo ya Mahakama ya Ilala ilitolewa na Hakimu Mkazi Mfawidhi, Martha Mpaze, baada ya kupitia ushahidi wa mashahidi wanne wa upande wa mashtaka ukiwamo ushahidi wa mama yake mzazi, Rafika Hawa Sidik.

Akizungumza nje ya mahakama Zarina aliishukuru Mahakama Kuu kumwona hana hatia, imemfutia adhabu ya mwaka mmoja jela ya kudaiwa kumtukana mama yake.



Katibu Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi, Daniel Chongolo akiwa pamoja Katibu wa NEC Siasa na Uhusiano wa Kimataifa, Kanali mstaafu Ngemela Lubinga (kulia) na Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi Mkoa wa Kigoma, Amandusi Nzamba (kushoto), wakiweka shada la maua katika kaburi la aliyekuwa Rais wa Burundi, hayati Petero Nkurunziza aliyefariki Juni 8, 2020 na kuzikwa Gitega nchini Burundi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Ulega: Tunataka maziwa yakuze ajira nchini

**Na Mbaraka Kambona, DODOMA**

NAIBU Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Abdallah Ulega, amesema serikali imejipanga kunakuwa na mazingira mazuri ya uwekezaji katika tasnia ya maziwa ili iweze kutoa fursa nyingi za ajira kwa vijana na kinamama nchini.

Alitoa kauli hiyo alipofanya ziara ya kukagua viwanda vya kuchakata maziwa, jijini Dodoma, mwishoni mwa wiki.

Alisema msimamo wa serikali ni kuona uwekezaji katika tasnia ya maziwa unashamiri ili zao hilo liweze kuongezewa thamani na kwa kufanya hivyo wananchi wengi watajipatia kipato kupitia mnyororo wa thamani.

"Tumepeleka mapendekezo ya kuondoa kodi nyingi ambazo zikiondoka zinakwenda kunawilisha tasnia ya maziwa, kwa mfano kodi zinazohusu vifungashio ili wawekezaji waweze kuzalisha kwa gharama nafuu na kukuza ajira kwa jamii," alisema.

Alisema serikali imedhamiria kukutana na wadau wa tasnia ya maziwa nchini kujadili nini kifanyike ili maziwa mengi yanayozalishwa na wafugaji yaende viwandani kwa ajili ya kuchakatwa na kuongezewa thamani, ili ajira nyingi ziweze kupatikana kwa vijana na kinamama.

"Mpaka hii leo maziwa mengi bado yanauzwa kienyeji huko mitaani jambo ambalo linasababisha upotevu mkubwa, kwa mfano ni asilimia tatu tu ya maziwa yote yanayozalishwa na wafugaji yanaenda viwandani ndiyo maana serikali inafanya jitihada kubwa kuondoa vikwazo vya kikodi ili mzalishaji wa kiwandani awe na uwezo wa kununua kwa bei nzuri kwa yule mfugaji ili washawishike kupeleka maziwa yao viwandani," alifafanua.

Alisema, serikali inakwenda kuweka vituo vya kukusanyia maziwa sehemu mbalimbali nchini, mwaka huu, imetenga bajeti ya kutosha kwa ajili ya kazi hiyo kwa kushirikiana na wadau ili maziwa mengi yaweze kukusanywa na kuingia viwandani.

Mkuu wa Wilaya ya Dodoma, Jabir Shekimweri, alisema katika jitihada za kuwezesha wafugaji kuinuka kiuchumi mkoani humo, kupitia mfuko wa kusaidia vijana, watu wenye ulemavu na wanawake wametoa mikopo kwa vikundi 12 ili wafanye ufugaji wa kisasa na kuzalisha maziwa mengi zaidi.

Alisema serikali ya mkoa ipo bega kwa bega na wawekezaji ili lengo la uwekezaji na ufugaji wenye tija waweze kuufikia kwenye makao ya nchi.

# Askofu TAG awakumbusha waumini ujenzi bora makanisa

**Na Julieth Mkireri,** KIBAHA

MAKAMU Askofu Mkuu wa Kanisa la Tanzania Assemblies of God (TAG), Dk. Magnus Mhiche, amesema wakati kanisa hilo likiwa kwenye mkakati wa maadhimisho ya miaka 13 ya moto wa uamsho, linatakiwa kuhubiri ujumbe huo ukiendana na majengo bora ya kufanyia ibada.

Alitoa rai hiyo mwishoni mwa wiki wakati akizindua Kanisa la Kibaha Christian Centre (KCC), Kibaha Mailimoja, akimwakilisha Askofu Mkuu wa TAG, Dk. Barnabas Mtokambali.

"Tuna mkakati wa 'miaka 13 ya moto wa uamsho, tunamtaka Yesu na nguvu zake' ni pamoja na uamsho wa kuona tuna majengo mazuri ya mahali pa kuabudia zamani tulikuwa tunachekwa sana watu walikuwa wanatusikitikia, lakini siku hizi mambo yamebadilika," alisema.

Alisema tangu Mungu alipomuumba mwanadamu, alitaka awe na ushirika naye na amuabudu, kuwa na majengo na sehemu maalumu ya kumuabudia haikuanzia sasa ilikuwapo tangu zamani.

Askofu wa Jimbo la Pwani Magharibi ambaye ni Mchungaji Kiongozi wa Kanisa hilo, Uswege Mwakisyala alisema ujenzi wa kanisa hilo ulianza mwaka 2017.

Askofu Mwakisyala alisema baada ya kukamilika kwa jengo hilo ambalo lililojengwa kwa nguvu za waumini na wadau wengine, litakuwa na uwezo wa kuchukua waumini 500 kwa wakati mmoja.

Askofu Mwakisyala aliwashukuru waumini kwa namna walivyojitoa kuhakikisha kanisa hilo linajengwa, aliwaomba waendelee kushikamana kufanikisha upatikanaji wa viti bora vinavyoendana na kanisa hilo.

Pia, aliwataka wakazi wa Kibaha kufika kufanya ibada katika kanisa hilo, huku akisema ukiwa na imani na Mungu ni suluhisho la kuepuka njia za mkato za kutaka mafanikio ya haraka.

"Sisi tunafanya kazi na serikali ambayo inatoa wito kwa watu kufanya kazi kujishughulisha, wapo vijana wengi wanafanikiwa wakiwa wanamwabudu Mungu hawa wanaopenda njia za mkato ni wale ambao wamemuacha Mungu," alisema Askofu Mwakisyala.

Mwakilishi wa Mkuu wa Wilaya ya Kibaha, Humphrey Mpute, alisema nyumba za ibada zinatakiwa kuhubiri amani na upendo kwa waumini wake.

HABARI KITAIFA

# Ripoti kutatua matatizo kwenye nafaka

**Na Faustine Feliciane**

SERIKALI imesema ripoti ya utafiti wa nafaka iliyofanywa chini ya Shirika la Umoja wa Mataifa la Chakula Duniani (WFP) itasaidia kutatua matatizo yaliyoko kwenye sekta hiyo.

Naibu Waziri wa Uwekezaji, Viwanda na Biashara, Exaud Kigahe, alisema ripoti hiyo iliyozinduliwa jijini Dodoma itaisaidia serikali kubaini maeneo yenye matatizo na kuyatatua kwa faida ya wachakataji wa nafaka.

"Lengo la serikali ni pamoja na kusimamia ubora wa viwanda nchini kwa kushirikiana na Shirika la Kuhudumia Viwanda Vidogo (SIDO), ili kusaidia wazalishaji na wasindikaji waendelee kuweka virutubisho kwenye uzalishaji wao," alisema Kigahe.

Alisema SIDO inapaswa kutenga maeneo tofauti yenye mazingira mazuri kwa wachakataji wa bidhaa za nafaka ili kuepuka uchafuzi wa mazingira.

Mwakilishi Mkazi na Mkurugenzi wa WFP Tanzania, Sarah Gordon-Gibson, akizungumza ripoti hiyo ya utafiti alisema, imebainika katika viwanda 33,000 vya usindikaji vyakula, asilimia 90 haviweki virutubisho.

Alisema utafiti huo uliendana sambamba na sensa ya wamiliki wa viwanda vya kusindika vyakula pamoja na kujua uwapo wa virutubisho.

"Utafiti huu ulilenga hasa kujua idadi ya viwanda, mahali vilipo, aina ya mashine zinazotumika na uwezo wake, lakini kubaini uwapo wa virutubisho ripoti inaonyesha viwanda vingi haviweki virutubisho," alisema Sarah.

Aliishukuru serikali kwa kusaidia kupata takwimu kwenye utafiti huo na kuwa wataendelea kushirikiana katika kuinua sekta hiyo ya usindikaji wa nafaka.




Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Dk. Dorothy Gwajima (kushoto), akipokea tuzo ya heshima kutoka kwa Mkurugenzi wa Ladies Talk Tanzania, Salome Sengo, kwa kutambua mchango wake katika kupambana na ukatili, kwenye hafla iliyofanyika mjini Morogoro juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wakulima walia na lumbesa, waiangukia serikali

**Na Thobias Mwanakatwe,**
IKUNGI

WAKULIMA kutoka kata saba zinazolima viazi vitamu wilayani Ikungi, mkoani Singida wamelalamikia kukithiri kwa vitendo vya baadhi ya wafanyabiashara na madalali kununua mazao yao kwa kutumia vipimo vya lumbesa visivyokubalika kisheria.

Malalamiko hayo yalitolewa juzi na viongozi wa Kata ya Puma, wakati Mkuu wa Wilaya ya Ikungi, Jerry Muro, alipofanya mkutano na madiwani, wenyeviti wa vijiji, vitongoji, watendaji na viongozi wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) kwa ajili ya kusikiliza kero zinazowakabili wananchi kwenye maeneo yao.

Kata zinazolima viazi katika Wilaya ya Ikungi ni Puma, Kituntu, Ihanja, Isyeke, Makiungo, Dung'unyi na Ikungi. Mwenyekiti wa Umoja wa Vijana wa CCM (UVCCM) Kata ya Puma, Hangida Ramadhani, alisema wafanyabiashara hao wamekuwa wakienda katika maeneo ya vijiji vya kata hizo na kutaka kuuziwa viazi kwenye magunia yaliyojazwa kupita uzito wa kawaida wa kilo 100.

Ramadhani alisema kwa ujazo wa lumbesa wakulima wamekuwa wakiuza viazi kwa Sh. 55,000 kwa ujazo wa zaidi ya kilo 200 badala ya kilo 100 unaokubalika kisheria.

Alisema kuwa ni vyema serikali ikaingilia kati tatizo hilo ili wafanyabiashara hao wasiendelee kuwanyonya wakulima wakati wanaponunua mazao na kuendelea kuwa maskini.

Alisema ununuzi wa mazao hayo kwa kutumia vipimo hivyo hauwanufaishi wakulima ambao hutumia nguvu kubwa na muda mrefu kuzalisha, matokeo yake huwapa faida wafanyabiashara.

Mkuu wa Wilaya ya Ikungi, Muro akijibu malalamiko hayo alisema serikali itashughulikia tatizo hilo na imeshaanza kwa zao la alizeti ambalo kulikuwa na ulaghai kama huo kwa wakulima.

Muro alisema tatizo kubwa lililopo ni kwa wakulima wenyewe ambao baadhi yao wamekuwa wakikubaliana na kuwauzia wafanyabiashara mazao yao kwa bei ya chini yakiwa bado yapo shambani kwa vipimo vya lumbesa ambavyo kimsingi havikubaliki.

"Njaa haina adabu ukiendekeza njaa utakufa maskini, hivi sasa tumekubaliana alizeti iuzwe kwa njia ya mnada, lakini wapo baadhi ya wakulima wanakwamisha."

# Mil. 540/- kumaliza kero upatikanaji maji Singida

**Na Thobias Mwanakatwe,**
SINGIDA

MAMLAKA ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Singida (SUWASA), imeanza kutekeleza mradi wa maji wa Sh. milioni 540 utakaokwenda kumaliza kero ya upatikanaji wa maji katika manispaa hiyo. Mhandisi wa Ufundi wa SUWASA Mkoa wa Singida, Richard Kasase, aliyasema hayo wakati wa uchimbaji wa kisima cha maji cha mradi wa Kata ya Mwankoko.

Alisema mradi huo utakapokamilika utaongeza kiwango cha upatikanaji wa maji katika manispaa hiyo kutoka lita za ujazo milioni 10 hadi kufikia lita milioni 12 kwa siku.

"Mahitaji ya maji kwa Manispaa ya Singida ni lita milioni 14, kwa hiyo pamoja na ongezeko hilo litafanya upatikanaji wa maji kufikia asilimia 85.7 kutoka asilimia 71.4 ya sasa," alisema. Kasase alisema mradi huo unatekelezwa kupitia fedha za Mpango wa Maendeleo kwa Ustawi wa Taifa na mapambano dhidi ya UVIKO-19. Alisema, ipo miradi mingine itakayoanza katika mwaka wa fedha wa 2022-/2023 ambayo ni wenye thamani ya Shilingi bilioni moja.

Kasese alitaja mradi mwingine ni wa uboreshaji wa huduma ya maji wa miji 28 wa fedha za mkopo wa masharti nafuu kupitia Benki ya India ambao ni mkubwa na utaongeza visima vinane na una kilometa 385.

Mkurugenzi Mtendaji wa SUWASA Mkoa wa Singida, Sebastian Warioba, alisema mabomba hayo yatalazwa kwenye eneo lenye urefu wa kilometa 3.8. Alisema mabomba hayo yenye kipenyo cha inchi tatu yana thamani ya Sh. milioni 83 na kuwa ni sehemu ya mradi wa maji wa Unyambwa ambao ukikamilika utamaliza kazi ya kuwapatia maji wananchi.

Alisema fedha za mradi huo zimetoka kwenye Mfuko wa Taifa wa Maji na katika mwaka huu wa fedha unaokwisha SUWASA ilikuwa imetengewa Sh. milioni 200 na mabomba hayo ni sehemu ya kiasi hicho cha fedha kilichotengwa kwa ajili ya manispaa hiyo.

Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni ya N & Ground Water Tanzania LTD ya Dodoma iliyopewa zabuni ya kuchimba eneo la Mwankoko, Mhandisi Naftal Mandi, aliishauri serikali kuwa miradi hiyo inakuwa na upotevu mkubwa wa fedha na eneo ambalo linakwenda kufanyika kwa mradi husika linatakiwa usanifu wa kitaalam kwa kuchimba shimo.

Mkuu wa Wilaya ya Singida, Mhandisi Mulagiri, alisema ili upatikanaji wa maji uongezeke kwa wananchi, serikali imetenga fedha za kuhakikisha kila mkoa unapata mitambo ya kuchimba mabwawa na bado wizara itakuwa na mitambo mingine ya kuchimba visima vya namna hiyo.



Irene Kamugisha ambaye ni miongoni mwa wanafunzi waanzilishi wa Shule ya Sekondari Baobab ya Mapinga Bagamoyo, akizungumza na wanafunzi wa shule hiyo alipotembelea shuleni hapo na waliokuwa wanafunzi wenzake. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

# Baobab yaanzisha kituo kulea yatima

**Na Joseph Mwendapole**

SHULE ya Sekondari ya Baobab ya Mapinga Bagamoyo, Mkoa wa Pwani, imeanzisha kituo cha kulelea yatima chenye uwezo wa kuchukua watoto 100.

Kituo hicho kilichoko shuleni hapo kimeanzishwa mwaka huu kwa lengo la kuwasaidia watoto wanaoishi kwenye mazingira magumu ambao wanahitaji kupata elimu na huduma zingine.

Hayo yalisemwa mwishoni mwa wiki na Meneja wa shule hiyo, Sophia Mawenya, wakati akizungumza kwenye kikao na wanafunzi waanzilishi wa shule hiyo walioitembelea kuangalia maendeleo yake.

Alisema shule hiyo ilianza ikiwa na wanafunzi 25 pekee, lakini kadri muda ulivyokwenda kasi ya wanafunzi ilizidi kuongezeka na kutanuka zaidi hali iliyowafanya waamue kuanzisha kituo cha kusaidia yatima kama shukrani kwa jamii.

"Jakaya Kikwete alikuja kuizindua shule hii mwaka 2007 akiwa Rais na baada ya hapo idadi ya wanafunzi ikaongezeka ghafla na kufikia 400 na tangu hapo tumepata wanafunzi wengi sana, hivyo mwaka huu tumeanzisha kituo cha yatima mkiona huko mitaani kwenu kuna watoto wanaohitaji msaada waleteni kwetu," alisema.

Aliwaasa wanafunzi wa shule hiyo kuwa kama wanataka mafanikio kwenye maisha yao, hawana budi kusoma kwa bidii na kujituma kwenye mambo ya msingi kwa kueleza kuwa hakuna mafanikio yanayoweza kuja bila mhusika kuyasumbukia.

"Tumewaleta hapa wanafunzi wenzenu waliosoma hapa na kupata mafanikio ili mjifunze kutoka kwao, hawa wana maisha mazuri kwasababu walikuwa na nidhamu na walikuwa wanajituma na hata kwenye vyuo walivyosoma sasa msiige mambo mnayoona kwenye TV mkayaleta shule," alionya.

Alitoa mfano kuwa yeye na mume wake walilazimika kuuza nyumba yao Sinza, jijini Dar es Salaam, ili kupata fedha za kuongeza madarasa kwenye shule hiyo hali iliyowashangaza watu wengi ambao walihoji sababu za kuuzwa kwa nyumba hiyo.

Sophia alisema, hata mshahara wake alioupata alipokuwa mtumishi wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM), alikuwa akiutumia kwenda kulipa mshahara kwa baadhi ya walimu na kununulia vifaa vya shule ili kuhakikisha shule hiyo inasimama.

"Hata aliyenunua nyumba yetu ya Sinza alitushangaa sana akauliza kwanini mmeamua kuuza hii nyumba, lakini kuna siku alimleta mtoto wake kusoma hapa alipotuona alishangaa akauliza hivi kumbe mliuza ile nyumba mje kujenga shule. Akasema mlifanya jambo la busara sana na mtoto wake alisoma hapa," alisema.

Mmoja wa wanafunzi wa mwanzo wa shule hiyo, Irene Kamugisha, alisema wameshangazwa na mazingira mazuri ya shule waliyoyakuta kwa kuwa walisoma shule hiyo ikiwa kwenye hali ngumu kutokana na kutokuwa na jengo hata moja la ghorofa.

"Kwa kweli tulipofika hapa tumeduwaa sana kwasababu haya maghorofa hayakuwapo wakati sisi tunasoma nawashukuru walimu na uongozi wa shule mimi nilijiendeleza na kuwa mhasibu na sasa hivi nafundisha masuala ya usimamizi wa fedha kwa watu na kampuni mbalimbali," alisema.

# Watakiwa kuunga mkono maendeleo sekta elimu

**Na Sabato Kasika**

WANANCHI wametakiwa kuunga mkono juhudi zinazofanywa na serikali kusaidia maendeleo kwenye sekta ya elimu, ili kuongeza ukuaji wa taaluma na ufaulu wa masomo.

Rai hiyo ilitolewa na Katibu Tawala wa Wilaya ya Ruangwa, mkoani Lindi, Inspekta Ayoub Pero, wakati akikabidhi vifaa vya shule kwa wanafunzi wa shule za msingi Dodoma na Liuguru.

Vifaa hivyo ni madaftari, kalamu za wino, kalamu za risasi, 'kaunta buku', rula, mikebe na vifutio, ambavyo vilitolewa na kikundi kiiitwacho 'Mpinda Family Mshikamano' cha mjini Ruangwa.

"Wakati huu ambao serikali inajenga madarasa katika shule zote nchini, wananchi hamna budi kuunga mkono juhudi hizo bila kujali uwezo wenu kiuchumi ili kusaidia maendeleo ya sekta ya elimu," alisema Inspekta Pero.

Katibu Tawala huyo alisema kikundi hicho kilichotoa vifaa vya shule ni mfano wa kuigwa na wadau wengine wa elimu, kwa kuwa vina mchango katika maendeleo ya elimu kwa wanafunzi.

Mwenyekiti wa kikundi hicho, Rashid Mpinda, alisema thamani ya vifaa hivyo ni Sh. milioni 2.5 ambavyo wamekabidhi katika shule mbili za msingi za Dodoma na Liuguru wilayani humo.

"Tulilenga shule hizi kwa sababu mimi na viongozi wenzangu katika kikundi hiki tulisoma katika shule hizi mbili, kwani kwa kawaida wema hua unaanzia nyumbani nasi tumeanzia tulikosoma," alisema Mpinda.

Alifafanua kuwa, lengo lao ni kusaidia shule mbalimbali wilayani humo na kwamba wameanza na hizo mbili na kisha wataendelea kadri ambavyo watafanikiwa kupata chochote.

Mwenyekiti huyo aliwaomba wazaliwa wa Ruangwa waliopo ndani na nje ya wilaya hiyo, kujitokeza kusaidia shule zote kwa hali na mali, ili wanafunzi wafikie malengo waliyojiwekea kwenye elimu.

Mwalimu Mkuu wa Shule ya Msingi Liuguru, Galus Ligambile, alisema msaada huo unasaidia baadhi ya wanafunzi wanaotoka katika familia zisizo na uwezo wa kuwanunulia vifaa vya shule.

# Wakulima ufuta walia uhaba pembejeo

**Na Julieth Mkireri,** KIBITI

BAADHI ya wakulima wa ufuta wameiomba serikali kuwapatia pembejeo za kilimo kama ilivyo katika korosho ili kuongeza uzalishaji. Walitoa ombi hilo juzi wilayani Kibiti wakieleza kuwa endapo watapatiwa ahueni ya pembejeo wakulima wengi watazalisha ufuta kwa wingi na watapata faida katika kilimo cha zao hilo.

Mmoja wa wakulima hao, Twaha Simba, alisema gharama kubwa kwenye ufuta ni dawa ambayo imekuwa ikinunuliwa mara kwa mara na kuomba iwapo serikali itasaidia kwenye pembejeo itakuwa imewasaidia wakulima.

Katibu wa Chama cha Ushirika Kibiti, Abdallah Kigumi, aliwaomba wakulima kuendelea kuzingatia maandalizi ya ufuta kuanzia shambani ili unapofika kwenye maghala ukiwa safi inawatangazia soko ndani na nje.

Akizungumza katika mnada uliofanyika Kibiti, Meneja wa Chama Kikuu cha Ushirika, Mkoa wa Pwani (CORECU) Mantawela Hamisi, alisema bei ya ufuta imekuwa ikipanda kwenye kila mnada kutoka Sh. 2,878 katika mnada wa kwanza hadi Sh. 3,222.32 katika mnada wa nne.

Alisema wanunuzi wa ufuta pia wanaongezeka kutoka 18 hadi 23, jambo ambalo linatoa hamasa kwa wakulima kuendelea kuongezeka kulima zao hilo.

Alisema kupitia minada hiyo wakulima sasa wanaona faida ya mazao yao kuuzwa katika mfumo wa stakabadhi ghalani, tofauti na ilivyokuwa awali kila unuzi kwenda kununua kwa mkulima kwa bei ambazo wakati mwingine inamkandamiza mkulima.

Nipashe
Spotika



WANAMICHEZO 6 WANAOINGIZA FEDHA NYINGI NJE YA UWANJA UK. 12-13



DYBALA

# WACHEZAJI HURU WA5 WANAOFAA SITA BORA EPL

**LONDON,** England

TIMU sita bora za Ligi Kuu England zinatarajiwa kuimarisha vikosi vyao msimu huu wa joto. Baada ya janga la COVID-19, klabu zimekuwa na tahadhari kidogo kuhusu kutumia fedha nyingi katika soko la uhamisho wa wachezaji. Kusajili mchezaji kwa uhamisho wa bure ni matarajio ya kuvutia sana kwa klabu yoyote.

Soko la wachezaji huru limejaa wachezaji kadhaa wa kiwango cha kimataifa msimu huu wa joto. Ni suala la muda tu kabla ya kupata klabu mpya na kuanza ukurasa mpya kwenye maisha yao ya uchezaji.

Makala haya inawaangalia wachezaji watano ambao wapo huru na wanaweza kufaa kwenye timu sita bora za Ligi Kuu England, EPL.

### #5 ISCO

Isco alikaa Real Madrid kwa misimu tisa. Amefurahia hali ya juu na chini na sasa anatarajiwa kuondoka katika klabu hiyo mwishoni mwa mwezi huu mkataba wake utakapokamilika. Isco ameshinda mataji matano ya Ligi ya Mabingwa Ulaya na matatu ya Ligi Kuu Hispania, LaLiga, akiwa na wababe hao wa Hispania.

Katika kilele cha nguvu zake, alikuwa mmoja wa viungo wa kati wabunifu zaidi barani Ulaya. Hata hivyo, ushawishi wake umepungua kwa kiasi kikubwa katika misimu michache iliyopita na hakuwa na nafasi kubwa pale Real Madrid katika msimu ya hivi karibuni.

Isco ana miaka 30 sasa, lakini bila shaka ana miaka michache zaidi ya kucheza kwa kiwango cha juu. Mhispania huyo angekuwa nyongeza nzuri kwa timu kama Tottenham Hotspur. Kikosi cha Antonio Conte kina ubora mwingi uwanjani, lakini kinahitaji sana mchezaji katika eneo la kiungo. Isco anaweza kuwa suluhisho kubwa kwao.

### #4 GARETH BALE

Gareth Bale bado ni nyota mwingine mwenye hadhi ya juu ambaye anatarajiwa kuondoka Real Madrid mwishoni mwa mwezi huu kama mchezaji huru. Katika mechi 258 za Los Blancos katika misimu nane, mchezaji huyo wa Wales amefunga mabao 106 na kutoa asisti 67.

Alishinda mataji matatu ya LaLiga na mataji matano ya Ligi ya Mabingwa Ulaya akiwa na Real Madrid. Bale amekuwa akichezea Real Madrid katika nyakati ngumu, lakini misimu yake michache iliyopita amekumbwa na matatizo ya majeraha.

Bale hakucheza sana kwenye kikosi cha Carlo Ancelotti msimu wa 2021-22. Alicheza mechi saba pekee katika michuano yote akiwa na Real Madrid msimu uliopita na kufunga bao moja.

Hata hivyo, Bale bado ni mchezaji mzuri na anaweza kuwa mchezaji bora kwa timu sita bora za Ligi Kuu England.

### #3 CHRISTIAN ERIKSEN

Christian Eriksen alijiunga na Brentford kama mchezaji huru Januari mapema mwaka huu. Mchezaji huyo wa kimataifa wa Denmark alithibitisha kwamba, bado ana kile anachohitaji kufanya katika Ligi Kuu ya England katika miezi michache aliyoichezea Brentford.

Tangu acheze kwa mara ya kwanza Brentford Februari 26, Eriksen alitengeneza nafasi 30 kwenye Ligi Kuu. Ni Kevin De Bruyne wa Manchester City (42) na Martin Odegaard wa Arsenal (38) pekee waliotengeneza nafasi nyingi zaidi kwa kipindi hicho.

Eriksen amekuwa akihusishwa na Manchester United na klabu yake ya zamani ya Tottenham Hotspur. Kwa mujibu wa David Ornstein, Mashetani Wekundu wametoa ofa kwa kiungo huyo wa Denmark. Eriksen mwenyewe alifichua katika mahojiano na Viaplay ya Sweden (kupitia Fabrizio Romano) kwamba, atafanya uamuzi juu ya mustakabali wake hivi karibuni. Alisema: "Nina chaguzi tofauti, ambazo tunazingatia, na kisha tunafanya uamuzi. Ningependa kucheza kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya. Ninajua jinsi inavyofurahisha, lakini sio muhimu kwangu."

### #2 PAULO DYBALA

Paulo Dybala anatarajiwa kuwa mchezaji huru mwishoni mwa mwezi huu. Amekuwa mmoja wa wachezaji muhimu wa Juventus katika muongo mmoja uliopita, lakini klabu na mchezaji huyo wameamua kuwa ni wakati wa kupeana mkono wa kwa heri.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Argentina amekuwa akihusishwa sana na Inter Milan. Lakini hauwezi kupuuza ukweli kwamba, anaweza kuwa nyongeza nzuri kwa moja ya timu sita bora za Ligi Kuu England. Dybala anaweza kuongeza ubunifu unaohitajika kwenye safu ya kiungo ya Tottenham Hotspur.

Anaweza pia kuwa nyongeza nzuri kwa Liverpool, ambayo alihusishwa nayo mnamo Machi. Tuttomercato iliripoti kwamba, Liverpool walikuwa wameanzisha mazungumzo ya kumsajili.

### #1 OUSMANE DEMBELE

Nyota wa Barcelona, Ousmane Dembele huenda akakosekana Camp Nou msimu huu wa joto. Klabu hiyo ya Katalunya imesikitishwa na matakwa ya mkataba mpya anaotaka Mfaransa huyo, kwa mujibu wa Mundo Deportivo na winga huyo anatarajiwa kuondoka klabuni hapo.

Kwa mujibu wa football.london, Chelsea wapo kwenye mazungumzo na kambi ya Dembele kuhusu uhamisho unaowezekana. Mfaransa huyo ndiye aliyeongoza kwa kutoa pasi za mabao (13) kwenye LaLiga msimu wa 2021-22 licha ya kucheza mechi 21 pekee.

Atakuwa nyongeza nzuri kwa wababe wa Ligi Kuu England kama vile Chelsea na Manchester United. Timu zote mbili zinatafuta winga wa kulia na Dembele ndiye anayefaa.

## ISIKUPITE

VINICIUS Junior atakuwa mmoja wanaongoza katika mbio za kuwania tuzo ya Ballon d'Or mwaka 2023, kwa mujibu wa Rivaldo. Mchezaji huyo wa kimataifa wa Brazil, alikuwa sehemu muhimu ya kikosi cha Real Madrid kilichoshinda taji la Ligi Kuu Hispania, LaLiga na Ligi ya Mabingwa Ulaya msimu wa 2021-22, akifunga bao pekee katika mchezo wa fainali wakati Los Blancos wakiichapa Liverpool.



# WANAMICHEZO SITA WANAOINGIZA FEDHA NYINGI NJE YA UWANJA


LEBRON JAMES

**LONDON,** England


NYOTA wa michezo wa leo ni alama za kimataifa. Wanafuatiliwa duniani kote na umaarufu huo hutafsiriwa kuwa bahati na pia wanakuwa soko kubwa.

**Ingawa wanamichezo bora zaidi duniani hupata fedha nyingi uwanjani, wengi huweka juhudi nyingi kudumisha vyanzo vya mapato yao. Wengi wa nyota wa michezo duniani ni wajasiriamali na mabalozi waliofanikiwa.**

Majina na sura zao zinatosha kutoa uaminifu kwa chapa za bidhaa mbalimbali.

Kwa mujibu wa jarida la Forbes, wanamichezo 50 wanaolipwa zaidi duniani walipata jumla ya dola bilioni 2.97 bila kujumuisha ushuru na ada za mawakala mwaka uliopita.

Makala haya inawatazama wanamichezo sita ambao waliopata mapato mengi zaidi kutokana na mikataba ya nje ya uwanja kwa msimu wa 2021-22.



#### #6 Cristiano Ronaldo – Dola Mil. 55

Cristiano Ronaldo ndiye mtu maarufu zaidi kwenye mitandao ya kijamii akiwa na wafuasi takriban milioni 708 kwenye Facebook, Instagram na Twitter. Ushawishi huu wa mitandao ya kijamii unamsaidia Ronaldo kujipatia fedha nyingi kupitia mikataba ya udhamini na kampuni kama Nike, Clear Shampoo na Herbalife.

Nguli huyo wa Ureno pia amemwaga fedha katika migahawa ya Tatel, ambayo hivi karibuni alifungua tawi jipya kule Beverly Hills nchini Marekani. Ronaldo pia ni balozi wa Zuju GP, programu inayokuja ya jumuiya ya soka ya kidijitali.

Ronaldo alipata dola milioni 55 kutokana na mikataba yake ya nje ya uwanja msimu wa 2021-22.

#### #5 Lionel Messi – Dola Mil. 55

Lionel Messi ana seti kubwa ya mikataba binafsi, ambayo faida yake kubwa na anapata dola milioni 20 kwa mwaka kwa ushirikiano na kampuni ya Socios. Pia ana mikataba na kampuni kama PepsiCo, Adidas na Budweiser.

Messi, ambaye aliweka rekodi ya kutwaa Ballon d'Or ya saba mwaka wa 2021, pia ni mwanamichezo wa kwanza kuwa balozi wa kampuni ya Hard Rock International. Anaendelea kuwa mmoja wa wanamichezo wenye ushawishi mkubwa kwenye sayari hii licha ya kutokuwa na msimu mzuri wa kwanza kule Paris Saint-Germain.



#### #4 Naomi Osaka – Dola Mil 58

Naomi Osaka kwa sasa ndiye mchezaji namba moja wa tenisi kwa wanawake. Ameshinda mataji manne ya Grand Slam na amekuwa mtu mashuhuri katika ulimwengu wa michezo. Osaka ni miongoni mwa wanamichezo wanaolipwa fedha nyingi zaidi duniani, akipata mapato ya nje ya uwanja.

Kwa mujibu wa Forbes, Osaka ana zaidi ya washirika 20 wa kampuni mbalimbali. Hizi ni pamoja na chapa maarufu duniani kama Nike, Mastercard na Louis Vuitton. Aliingiza kiasi cha dola milioni 58 kati ya Mei 2021 na Mei 2022.

Osaka ndiye mwanamichezo wa kike anayelipwa fedha nyingi zaidi duniani, kwa sasa akipata kiasi cha dola milioni 58 kwa mwaka.

#### #3 Tiger Woods – Dola Mil 68

Tiger Woods sasa ana utajiri wa angalau dola bilioni moja. Anaungana na Michael Jordan na LeBron James kama wanamichezo pekee kufikisha mapato ya dola bilioni. Tiger Woods ni mshindi mara 15 wa mataji makubwa na ana mikataba yenye faida kubwa.

Woods anaudhamini kwa chapa za Nike, Monster Energy, Gatorade na TaylorMade miongoni mwa zingine. Pia amebadilisha vyanzo vyake vya mapato na anamiliki TGR Design, kampuni ya kubuni gofu pamoja na TGR Live, mpango wa kutengeneza matukio ya moja kwa moja. Pia ana mgahawa unaoitwa The Woods.

Woods pia amewekeza fedha kwenye kampuni za Full Swing, Heard na Popstroke.

#### #2 LeBron James – Dola Mil 80

LeBron James hakuweza kuiongoza Los Angeles Lakers kwenye mchujo msimu huu, lakini hilo halijaathiri hali yake ya kiuchumi nje ya uwanja. James amepata dola milioni 80 kupitia mikataba ya nje ya uwanja kati ya Mei 2021 na Mei 2022.

Alipata fedha nyingi kupitia kampuni anazozitangaza kama vile The Shop, YouTube, HBO. James alionekana na kutoa pamoja filamu ya vichekesho ya Marekani ya 2021 ya Space Jam: A New Legacy.

Nyota huyo mwenye umri wa miaka 37 alipata fedha nyingi zaidi baada ya kuuza hisa kubwa kwenye kampuni ya SpringHill. James pia alitia saini mkataba na kampuni ya Crypto.com, Januari 2021.

Mwanamichezo huyo pia amemwaga fedha kwenye kampuni ya Tonal, inayohusika na biashara ya vifaa vya mazoezi vya nyumbani, na StatusPro.

#### #1 Roger Federer – Dola Mil 90.7

Roger Federer ni sawa na darasa na uzuri. Ingawa majeraha yalimfanya akose kwa muda mwingi wa 2020 na 2021, vyanzo vyake vya mapato havikuisha. Federer ana mikataba na kampuni za Rolex na Uniqlo na amepata fedha nyingi kupitia kampuni ya viatu ya Uswizi ya On.

Federer ameshinda mataji 20 ya Grand Slam na anatazamwa na wengi kama mojawapo ya mchezaji bora zaidi wa tenisi wa wakati wote. Alipata dola milioni 90.7 kama mapato kupitia mikataba ya nje ya uwanja kati ya Mei 2021 na Mei 2022.

Federer, mchezaji wa tenisi anayelipwa zaidi duniani aliingiza dola milioni 90.7 katika miezi



12 iliyopita, lakini ni dola milioni 0.7 pekee zilizopatikana kutokana na kucheza tenisi.

## Nukuu

"Ni wakati muhimu. Hakuna maana kwa mtu yeyote kujaribu kujifanya vinginevyo," alisema Klopp akiiambia tovuti ya klabu. Mmoja wa wachezaji bora kabisa wa Liverpool anaondoka na lazima tukubali hili. Anaondoka na shukrani zetu na upendo wetu. Anaondoka na hadhi yake kati ya magwiji waliohakikishiwa. Na ndio anaondoka katika wakati ambapo yeye ni mmoja wa wachezaji bora katika soka la dunia." **Jurgen Klopp akimzungumia Saido Mane ambaye ameondoka Liverpool na kujiunga Bayern Munich**



"NI vigumu kutaja wachezaji wanaopewa nafasi kubwa kwenye Ballon d'Or wakati msimu haujaanza, lakini namuona Vinicius Junior hatakosekana pamoja na Kylian Mbappe, Kevin De Bruyne na wengine." **Rivaldo**



"KAMWE usiseme hapana, kama kocha, hakuna klabu 50 ambazo ninaweza kwenda. Kuna uwezekano wa klabu mbili au tatu." **Zinedine Zidane.**





Straika mzawa tishio kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara, George Mpole ambaye taarifa zinasema kuwa klabu ya Simba inamwinda.

# TETESI USAJILI 10 WACHEZAJI WA KIBONGO

**Na Adam Fungamwango**

Ni msimu wa usajili ambao hauna tetesi nyingi za wachezaji wa Kitanzania kuhitajiwa na klabu nyingine, hasa kubwa.

**Miaka kadhaa nyuma mida hii kungekuwa na patashika nguo kuchanika kwa klabu kubwa kama za Simba, Yanga na hata Azam kugombania, kunyang'anyana wachezaji wa Kibongo.**

Msimu huu pilikapilika zimehamia zaidi kwa wachezaji kutoka nje ya nchi. Ndiyo maana tunawasikia kina Stephane Aziz Ki, Moses Phiri, Victorien Adebayor na wengine.

Siyo kwamba huko nyuma hakukuwa na tetesi au kugombea wachezaji wa kigeni, ila hata wachezaji wa Kitanzania nao walizitia hekaheka klabu hizi kubwa.

Wachezaji kama Malimi Busungu, Said Bahanuzi, John Bocco, Erasto Nyoni, Mohamed Hussein 'Tshabalala', Aggrey Morris, Bakari Mwamnyeto, Shomari Kapombe, na wengine kwa misimu tofauti walitikisa kwenye vipindi tofauti.

Kwa sasa siyo hivyo. Tayari Mabingwa wa Tanzania Bara Yanga wameshasema kuwa hawatosajili mchezaji yoyote wa Kitanzania, badala yake wanaongeza wachezaji wa kigeni watatu au wanne tu ili kukiimarisha kikosi chao.

Kwa hiyo tetesi chache za wachezaji wa Kitanzania kutakiwa na timu kubwa, zimebaki kwa Simba na Azam tu. Mwandishi wa makala haya anakusanya majina ya wachezaji wachache ambao angalau nao wanatajwa kuwaniwa na klabu hizi kwenye Ligi Kuu ya msimu ujao.

### 1. George Mpole - Simba

Ndiye straika pekee wa Kitanzania aliye midomoni mwa mashabiki wa soka, watangazaji, wachambuzi na kwenye kalamu za waandishi wa habari.

Mpaka sasa anaongoza kwenye kufumia nyavu akiwa na mabao 16 sambamba na Mkongomani, Fiston Mayele wa Yanga.

Ametoa pasi za mabao nne, huku Mayele akiwa na 'assist' tano.

Kutokana na umahiri wake wa kufumania nyavu, si akiwa na timu yake ya Geita Gold bali hata timu ya taifa, Taifa Stars, anatajwa kuhitajika na klabu ya Simba.

Zipo taarifa kuwa viongozi wa Simba kwa sasa wanahangaika na wako kwenye hatua za mwisho kuinasa saini yake, ili kuziba pengo la straika wa Kitanzania, John Bocco, mfungaji bora wa msimu uliopita ambaye msimu huu hakuwa vizuri.

### 2. Nassor Kapama - Simba

Wengi wanamfahamu kama ni strika mahiri akiwa na timu mbalimbali ikiwamo Ndanda FC miaka ya nyuma wakati iko Ligi Kuu.

Hata misimu kadhaa akiwa na Kagera Sugar alikuwa akicheza kama mshambuliaji. Kwa sasa anaonekana amebadilisha namba. Kuna wakati anacheza kama kiungo mkabaji, na beki wa pembeni, nafasi ambazo amezicheza kwa ustadi mkubwa hata kushangaza wengi.

Ameivutia klabu ya Simba ambapo zipo taarifa au tetesi kuwa tayari wameshamaliza naye. Simba haitomchukua kama straika, ingawa kuna wakati ikihitaji anaweza kuwasaidia kwa hilo.

Walivutika zaidi na nafasi yake ya sasa ya beki, ndiyo iliyowafanya Simba mate yawatoke.

### 3. Nathaniel Chilambo-Azam

Awali ilisemekama kuwa Simba ilimhitaji. Lakini baadaye ni kama kibao kikageuka. Azam nao inadaiwa iliingiza mkono.

Habari zinasema kuwa ana asilimia nyingi tu za kutua maeneo ya Chamazi kwenda kukipiga na Azam FC, ambao wameonyesha nia naye ya dhati.

Huyu ni beki kijana wa Ruvu Shooting, ambaye ameonyesha uwezo mkubwa msimu huu, ukiwa ni wa kwanza kwake kwenye Ligi Kuu.

### 4. Cleophace Mkandala-Azam

Kiungo huyu mshambuliaji wa Dodoma Jiji ananukia kwenye mitaa ya Chamazi kwenda kujiunga na Azam FC.

Mchezaji huyu ambaye alianzia karia yake ya soka kwenye kikosi cha pili cha Yanga, alimkosha kocha wa zamani wa Simba Didier Gomes kwenye mechi za mzunguko wa kwanza wa Ligi Kuu kiasi cha kupendekeza asijiliwe mwishoni mwa msimu, lakini aliondoka.

Bado Simba walikuwa kwenye rada, lakini baadaye tetesi hizo zikapotea, na za kutakiwa na Azam zikaibuka. Inasemekana tayari Azam imeandaa mkataba wa miaka miwili kwa ajili ya mchezaji huyo.

### 5. Dickson Mhilu-Simba

Ni ndugu yake Yusuph Mhilu ambaye anakipiga klabu ya Simba. Tetesi zinasema huenda Dickson Mhilu akmfuata kaka yake kwenye klabu hiyo, baada ya kuvutiwa sana na uwezo wake, akicheza kama beki wa pembeni.

Simba inataka kuimarisha eneo la pembeni, kulia na kushoto wanakocheza Kapombe na Tshabalala kutokana na wachezaji wao kutumika kwa muda mrefu bila kupumzika, hivyo kuwa wakati wanashuka viwango kwa sababu ya uchovu.

### 6. Said Ndemla-Azam

Kwa sasa anaichezea Mtibwa Sugar kwa mkopo, akitokea kwenye klabu ya Simba. Inaonekana ni kama vile timu yake ya zamani haina mpango naye, hivyo tetesi zinasema kuwa huenda akatua Azam FC.

Azam inataka kumchukua kiungo mshambuliaji huyo ili kuziba pengo la Salum Aboubakar 'Sure Boy' ambaye alitimkia Yanga kipindi cha dirisha dogo la usajili.

### 7. David Kameta-Simba

Klabu ya Simba ilimtoa kwa mkopo msimu uliopita kwenye klabu ya Biashara United msimu mmoja uliopita, na msimu huu bado ni mali ya Wekundu wa Msimbazi, lakini akiichezea Geita Gold kwa mkopo pia.

Beki huyo wa pembeni kulia maarufu kama Duchu, amekuwa kwenye kiwango cha hali ya juu msimu huu, kiasi kwamba klabu yake ya zamani ina mpango wa kumrejesha tena.

### 8. Ibrahim Ajibu-Singida Big Stars

Tetesi zinasema huenda akaachana na Azam FC mwishoni mwa msimu na majeshi yake kupeleka kwenye klabu ya Singida Big Stars ambayo tayari imepanda Ligi Kuu, ikiwa imebadilishwa jina kutoka DTB. Ajibu alijiunga na Azam FC msimu huu baada ya makubaliano ya kuvunja mkataba wa klabu ya Simba kufanyika.

### 9. Abdul Selemani 'Sopu'-Simba

Winga huyu machachari, ndiye kwa kiasi kikubwa aliyefunga mabao ambayo yaliibakisha katika daraja Coastal Union msimu uliopita. Na msimu huu ameibeba mno timu hiyo kufikia hapo ilipofika, ikiwa haina 'stresi' za kushuka daraja tena kama ilivyokuwa kwenye mzunguko wa kwanza ambapo ilikuwa inaburuza mkia.

Amepachika mabao saba mpaka sasa kwenye Ligi Kuu. Tetesi zinasema kuwa Simba inamhitaji kwa udi na uvumba, ikitaka kurejesha zao lake.


Abdul Selemani 'Sopu' alicheza kwenye kikosi cha vijana cha Simba, lakini baadaye akatolewa kwa mkopo kwenye klabu ya Ndanda wakati huo ikiwa Ligi Kuu, kabla ya kwenda Coastal Union.

### 10. Gadiel Michael-Singida Big Stars

Inaelezwa kuwa Gadiel ni mmoja wa wachezaji ambao wanaweza kupewa mkono wa kwaheri utakapomalizika msimu.

Tetesi zinasema kuwa huenda akatimkia kwenye klabu ya Singida Big Stars, timu ambayo inaonekana kujizatiti ili kuwa timu ya kutisha msimu ujao.

**JE, WAJUA?**



WAKALA wa zamani wa Neymar, Wagner Ribiero amesema kuwa Mbrazil huyo hayuko tayari kuondoka Paris Saint-Germain kwa vile bado ana ndoto ya kutwaa ubingwa wa Ligi ya Mabingwa Ulaya akiwa na mabingwa hao wa Ufaransa.



# H'shauri yatoa bil. 1.5/- mikopo makundi maalum

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

HALMASHAURI ya Jiji la Dodoma imetoa Sh. bilioni 1.5 kwa ajili ya mikopo ya vikundi vya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu.

Mkurugenzi wa jiji hilo, Joseph Mafuru, aliyasema hayo jana kwenye hafla ya kukabidhi hundi hiyo ya mikopo kwa vikundi hivyo.

Alisema fedha hizo zimeelekezwa kwa kinamama wajasiriamali, vijana waendesha bodaboda na bajaji pamoja na watu wenye ulemavu.

Alisema utoaji huo wa mikopo ni mwendelezo wa jiji katika kuhakikisha asilimia 10 ya mapato yake inawakopesha wajasiriamali.

Mafuru alisema fedha hizo zimetolewa na serikali zitumike kwa malengo yaliyokusudiwa ikiwa na pamoja kurejesha kwa wakati ili wengine wapatiwe mikopo.

"Mikopo hiyo ninawaomba vikundi vyote vilivyopewa, tumieni kwa ajili ya kujiletea maendeleo ya kiuchumi, naomba msielekeze kwenye anasa," alisema.

Kwa upande wake, Mkuu wa Wilaya ya Dodoma, Jabir Shekimweri, alisema ili mikopo hiyo iwe na manufaa kwao wanatakiwa kuitumia kwa malengo ili kurejesha kwa wakati.

Aliwataka wajasiriamali hao kuwa wabunifu ili kuingia kwenye ushindani wa masoko na kutengeneza bidhaa zao kwa ubora.

Aliwataka vijana waendesha bodaboda kutotumia fursa hiyo kwa kujihusisha na vitendo vya unyang'anyi na kamwe serikali haitawaacha.

"Kuna wengine waendesha bodaboda wamezikunja vibati vya namba za usajili na wengine kuondoa vioo suala ambalo linaloonyesha sio waaminifu watu hao," alisema.

Aliwataka kutumia mikopo hiyo kujikwamua kiuchumi na kurejesha kwa wakati ili kusaidia wengine.




Mkuu wa Wilaya ya Dodoma, Jabiri Shekimweri (mwenye koti jeusi), akisalimiana na kinamama wakiwamo vijana na watu wenye ulemavu kwenye makabidhiano ya hundi ya mfano ya mkopo wenye thamani ya bilioni 1.512/- kwa ajili ya vikundi hivyo iliyofanyika jijini Dodoma jana. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# Maofisa Elimu wapewa jukumu kuinua elimu

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

WAZIRI wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Adolf Mkenda, ameagiza maofisa elimu maalum kuhakikisha wanainua elimu kwenye maeneo yao.

Prof. Mkenda alibainisha hayo juzi jijini hapa alipokuwa akifungua mkutano mkuu wa pili wa Umoja wa Maofisa Elimu Maalum Tanzania.

Alisema sekta ya elimu nchini bado inakabiliwa na vikwazo mbalimbali ambavyo serikali inaendelea kuvifanyia kazi ili kuvipunguza.

"Lazima tumuunge mkono mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan kwa jitihada anazozifanya, muwe wabunifu kila siku yenu ya kazi iwe ni siku ya kupunguza changamoto zilizoko katika sekta hii ya elimu nchini," alisema.

Naye Naibu Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), anayeshughulikia elimu, Dk. Charles Msonde, aliwataka maofisa hao kuhakikisha watoto wenye mahitaji maalum wanapata elimu bila kikwazo.

Alisema maofisa hao wanajukumu la kupita na kukagua mara kwa mara shule ambazo watoto hao wanasoma ili kubaini kama wanachopatiwa ni kile wanachokistahili kukipata.

"Mmefanya kazi ya kuwabaini na kuwaandikisha watoto wenye mahitaji wengi nchini, lakini hilo halitoshi lazima mhakikishe kuwa wanapata elimu wanayostahili kupata sio kubainisha tu na kuwandikisha, tembeleeni shule kuona kama vile wanavyostahili wanavipata," alisisitiza Dk. Msonde.

Alisema ni wajibu wa serikali kuona watoto wenye mahitaji maalum wanapata elimu bora wanayostahili na sio vinginevyo.

"Lazima tufuatilie kama wanasoma kinachostahili, wanachofundishwa ni sahihi kama tusipo fuatilia matokea ya mitihani ya mwisho yatatuumbua kwani pamoja na kuandikisha watoto wengi, lakini matokeo bado ni mabovu kila mwaka."

"Umoja huu ulete tija kwa watoto wetu wanaosoma elimu maalum tujielekeze katika taaluma badala ya kuwa wanaharakati, nadhani mnanielewa ninaposema uanaharakati tusifike huko siku zote taaluma haina ubabaishaji mie nitawapa ushirikiano wa kutosha siku zote milango yangu itakuwa wazi," alisisitiza.

# Tanzania kuendeleza ushirikiano kiutafiti na DRC

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

WAZIRI wa Kilimo, Hussein Bashe, amesema serikali itaendelea kushirikiana na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (DRC) kufanya utafiti, kubadilishana utaalamu na kuimarisha soko la mazao mbalimbali.

Bashe alitoa kauli hiyo mwishoni mwa wiki alipokuwa akizungumza na ujumbe kutoka Kongo ulioongozwa na Gavana wa Jimbo la Katanga, Jacques Kyabula Katwe, ambao upo nchini kwa ziara ya siku tatu kufuatilia ushirikiano na Tanzania katika nyanja mbalimbali ikiwamo kilimo.

"Ili kuhakikisha Kongo inanufaika na mazao mbalimbali kutoka Tanzania serikali inaendelea kuimarisha ujenzi wa maghala mbalimbali ambapo kwa sasa Tanzania kupitia Taasisi ya Utafiti wa Kilimo (TARI), imejipanga kutoa mafunzo ya kiutaalamu kwa wataalamu wa kilimo kutoka ukanda wote wa Mashariki ya Kongo pamoja na kuiwezesha Kongo," alisema.

Alisema Tanzania itaingia makubaliano ya kisheria na ukanda mzima wa Mashariki mwa Kongo kufanya shughuli za kilimo.

"Tanzania inaenda kufungua maghala mengi zaidi kwa ajili ya kuhifadhi mazao ya aina mbalimbali ambayo yanahitajika zaidi nchini DRC na wafanyabiashara wa nchini hawataingia mitaani kuuza mazao ila Wakongo wenyewe watanunua kwenye maghala na kwenda kuuza kwa watu wao," alisema Bashe.

Kwa upande wake, Gavana wa Jimbo la Katanga, Jacques Kyabula Katwe, alisema kuwa Jimbo la Katanga linavutiwa na uwezo wa Tanzania katika shughuli mbalimbali za kilimo.

Alisema atahakikisha kuwa biashara ya chakula kutoka Tanzania inazidi kuimarika na wataendelea kushirikiana ili kuwanufaisha wakulima wa Katanga.





# Mradi mkubwa wa maji watarajiwa Rungwe

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

ZAIDI ya Sh. bilioni 300, zinatarajiwa kutumika katika utekelezaji wa mradi mkubwa wa maji kutoka Mto Kiwira Wilaya ya Rungwe, mkoani hapo baada ya kukamilika kwa upembuzi yakinifu na usanifu wa mradi huo.

Mkurugenzi Mtendaji Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira, Mkoa wa Mbeya, Gilbert Kayange, aliyasema hayo juzi wakati akizungumzia hatua zilizofikiwa katika utekelezaji wa mradi huo mkubwa wa maji ambao utahudumia Jiji la Mbeya, Wilaya ya Rungwe na baadhi ya sehemu kwenye Wilaya ya Chunya.

Alisema mradi huo ukikamilishwa utazalisha lita za maji milioni 125 kwa siku na lengo la serikali ni kuhakikisha mama anatuliwa ndoo kichwani kwa kumwondolea adha ya kutembea umbali mrefu kufuata huduma hiyo mbali na makazi yake.

"Usanifu wa mradi huo tayari umefanyika na tunategemea mwezi Septemba makandarasi kuanza kutekeleza mradi huo ambao utakamilika ndani ya miaka miwili," alisema CPA Kayange.

Alisema mradi huo utasaidia kuondokana na adha ya upatikanaji wa maji, kwa sasa katika Jiji la Mbeya uzalishaji wa maji ni lita milioni 51,500 kwa siku huku uhitaji ukiwa ni lita milioni 90,000 kwa siku.

Kayange aliongeza kuwa wakati wanasubiri suluhu ya kudumu kuhusu upatikanaji wa maji wameweka mikakati ya kuongeza uzalishaji wa majisafi na salama na ifikapo June 30, mwaka huu wataongeza usambazaji wa maji na kufikia lita milioni 15.

Baadhi ya wafanyabiashara jijini hapa akiwamo Josephat Hobokela, alisema utakapoanza mradi wa Kiwira itakuwa fursa kwao kwa kuwa watapata wateja wengi wa vifaa vya ujenzi na wamejipanga kunufaika na ujenzi wa mradi huo.

# Zaidi ya bil. 175/- kutumika mradi kurejesha ikolojia

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

SERIKALI imepanga kutumia Dola za Kimarekani milioni 75.5 (sawa Sh. bilioni 175.6) kwa ajili ya mradi wa kurejesha Ikolojia kwenye Bonde la Mto Ruaha na Ziwa Rukwa, kati ya fedha hizo Dola milioni 11 zimetolewa na Mfuko wa Mazingira Duniani (GEF).

Kauli hiyo ilitolewa mwishoni mwa wiki na mratibu wa mradi huo kutoka ofisi ya Makamu wa Rais Mazingira, Dk. Damas Mapunda, alipokuwa akiwajengea uwezo watendaji wa halmashauri saba kutoka mikoa mitano iliyoingizwa kwenye utekelezaji wa mradi huo.

Alisema mradi huo ni wa kipindi cha miaka mitano na utakuwa na lengo la kurejesha ikolojia iliyoathiriwa na matumizi ya kilimo pamoja na ufugaji hususani kwenye Wilaya ya Mbarali.

"Mradi huu unalenga kuyafikia maeneo yote yaliyoathiriwa na shughuli mbalimbali za kibinadamu kama vile kilimo, ufugaji na uvuvi na kusababisha ikolojia kupotea, tutahakikisha tunarudisha na kunusuru upotevu wa maji na uoto wa asili, alisema Dk. Mapunda.

Vile vile, katika mradi huo watarejesha uoto wa asili, maji kwenye mito na kunusuru Bonde la Usangu, wilayani Mbarali ambalo limepungua kutoka kilometa za mraba 322 mpaka 84 katika kipindi cha kuanzia mwaka 1999 hadi 2006.

Alisema katika kukabiliana na uharibifu wa mazingira, wameweka mikakati ya kujenga skimu za umwagiliaji kwenye maeneo ambayo mradi utapita ili kuepuka athari za kiuchumi kwa jamii ambayo inaegemea maji ya mito na mabonde kwa ajili ya kilimo cha umwagiliaji katika mabonde ya Ruaha Kuu na Rukwa.

Dk. Mapunda alisema, asilimia 15 ya maji yanayozalishwa Bonde la Mto Ruaha yanategemewa kuzalisha umeme katika Bwawa la Mwalimu Nyerere na kuna kila sababu ya kuhakikisha maji yanalindwa ili kuchochea uchumi wa nchi.

Akizungumzia mradi huo, Katibu Tawala Msaidizi anayeshughulikia Uchumi na Uzalishaji Mkoa wa Mbeya, Said Madito, alisema utekelezaji wa mradi huo utawahusisha watendaji kuanzia ngazi za vijiji na kata ili kupata matokeo mazuri.

Alisema, halmashauri zinapaswa kusimamia kikamilifu utekelezaji wa mradi huo kwa kuhakikisha elimu juu ya utunzaji wa mazingira, ikolojia na uoto wa asili vinatunzwa kwa manufaa ya kizazi cha sasa na baadaye.

Kwa upande wake, Mkurugenzi Msaidizi, Idara ya Mazingira kutoka Ofisi ya Makamu wa Rais, Faraja Ngalageza, alisema mradi huo utafanya kazi kubwa kurejesha ardhi zilizoharibiwa kwa shughuli za kijamii. Mradi huo unaratibiwa na ofisi ya Rais Makamu wa Rais, Mazingira na utahusisha mikoa ya Mbeya, Iringa, Njombe, Katavi na Rukwa na kwamba kwa sasa wameelezwa maeneo yatayopitishwa na mradi huo ili wakasimamie vyema utekelezaji kwa kipindi cha miaka mitano.




Mwakilishi wa Kampuni ya Pandahill Tanzania inayojihusisha na uchimbaji wa madini ya Niobium mkoani Mbeya akiwaonyesha wanahabari sampuli za madini hayo jana, katika kongamano la nishati na madini linalofanyika jijini Mbeya. **PICHA: GRACE MWAKALINGA**

# Waiomba serikali kuwajengea barabara walioianza kwa mikono

**Na Grace Mwakalinga,** RUNGWE

WANANCHI wa vijiji vya Kyobo Juu na Kyobo Chini, vilivyoko Kata ya Ikuti, wilayani Rungwe, wameiomba serikali kuwasaidia kujenga barabara yao waliyoilima kwa mikono miaka iliyopota ili magari yaweze kupita.

Wakizungumza kwenye mkutano wa hadhara ulioandaliwa na Mkuu wa Wilaya Rungwe, Dk. Vicent Anney, wananchi hao walisema kuwa barabara pekee inayoingia kwenye vijiji hivyo waliilima wenyewe kwa mikono miaka mingi iliyopita na haijawahi kukwatuliwa na greda.

Deus Mwaijumba, alisema kwa namna barabara hiyo ilivyolimwa na wazee wao miaka mingi iliyopita, magari hayawezi kupita na kuvifikia vijiji vyao na kuomba msaada wa serikali iiboreshe ili iweze kupitika.

"Barabara hii ambayo ndiyo inaingia kwenye vijiji vyetu vya Kyobo Juu na Kyobo Juu haijawahi kutumiwa na magari tangu nchi ipate Uhuru, hii ni kwa sababu ililimwa kienyeji na wazee wetu kwa kutumia jembe la mkono miaka mingi iliyopita, tunaomba sasa serikali itusaidie kuilima kwa greda ili magari yapite na hata kufika kwenye vijiji vyetu," alisema Mwaijumba.

Alisema katika vijiji hivyo wanazalisha mazao mengi ya biashara na chakula kama vile ndizi, iliki, kahawa, magimbi na mihogo, lakini hawawezi kuyasafirisha kwa wingi kwenda kuyauza.

"Tunayo mazao yetu tunayolima kwa wingi, ingawa tunajua yana soko kubwa nje ya vijiji vyetu, lakini tunashindwa kuyasafirisha kwa wingi na hata wanunuzi wanashindwa kuja kuyanunua kwa sababu hakuna barabara, badhi yetu tunalazimika kuyabeba kichwani kwenda kuyauza ili tupate fedha za kujikimu, tunaomba tusaidiwe barabara kuondokana na kero hizi," alisema Mwaijumba.

Kwa upande wake, Lucia James, alisema ukosefu wa barabara pia unathari kubwa kwa wanawake hasa wajawazito wanapohitaji kujifungua pale wanapotaka kwenda kwenye vituo vya afya.

Alisema usafiri pekee unaowasaidia wajawazito kwenda kujifungua kwenye vituo vya afya ni pikipiki, aliodai kuwa sio rafiki kwa baadhi yao wenye matatizo ya uzazi. Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Rungwe, Mpokigwa Mwankuga, aliomba msaada wa ujenzi wa barabara hiyo, kwa serikali kuu kutenga bajeti ya kuwasaidia wananchi hao katika mwaka ujao wa fedha.

Mwakilishi wa Meneja wa Wakala wa Barabara za Mijini na Vijijini (TARURA), Wilaya ya Rungwe, Mhandisi Senyange Kayoka, alisema jukumu la TARURA ni kufungua barabara kwenye maeneo yote ili wananchi wazitumie kwa shughuli za maendeleo.

Aliahidi katika mwaka ujao wa fedha barabara hiyo itakuwa ya kwanza kuingizwa kwenye bajeti ya TARURA ili iweze kujengwa na kumaliza kero ya wananchi hao.

Akizungumza na wananchi hao, Mkuu wa Wilaya ya Rungwe, Dk. Anney alisema atasimamia kikamilifu kuhakikisha barabara hiyo inapitika kwa gari kwa manufaa na maendeleo ya wananchi wa vijiji hivyo.

Alisema kuwa barabara hiyo ikifunguka anaamini wananchi hao watapata maendeleo ya haraka kwa vile ni wazalishaji wazuri wa mazao ambayo yanapendwa na yenye soko la uhakika ndani na nje ya Wilaya ya Rungwe.





Mtumwa Fadhil Hamad mkaazi wa Kijiji cha Makangale Pemba ni miongoni mwa wanufaika wa kaya maskini katika mfuko wa TASAF, akichora mkoba kwa ajili ya kuupaka rangi baada ya kuutengeneza. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Mabadiliko tabianchi yaathiri ushoroba wa wanyama

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MTAALAMU wa mipango ardhi na bioanuwai, katika mradi wa Tuhifadhi Maliasili unaofadhiliwa na Shirika la Misaada la Marekani (USAID), Joseph Olila, amesema mabadiliko ya tabianchi Tanzania yameathiri njia za wanyama pori (ushoroba) ambazo huzitumia kutoka sehemu moja kwenda zingine.

Aliyasema hayo wakati akitoa mada kuhusu wajibu wa serikali kulinda ushoroba wa wanyamapori katika mafunzo ya waandishi wa habari yaliyoandaliwa na Chama cha Waandishi wa Habari za Mazingira Tanzania (JET), yaliofanyika kwa njia ya mtandao.

Alisema kutokana na athari hizo kumesababisha wanyamapori kutoka katika makazi yao na kuhujumu wananchi pamoja na mali zao ikiwamo mazao mashambani.

Alisema njia hizo huzitumia wanyamapori kwa usalama wao kwa mahitaji mbalimbali ikiwamo kupata chakula kwa kutoka eneo moja kwenda lingine.

Alisema athari hizo pia zimesababisha kuwapo kwa migongano mingi kutoka na sababu mbalimbali ikiwamo njia wanazotumia pia hutumiwa na binadamu.

Aidha, alisema njia hizo zikihifadhiwa na kulindwa zitasaidia kupunguza uwezekano wa wanyamapori kuingiliwa katika mfumo wao wa maisha, pia katika hali mbaya ya kimazingira kutumia njia hizo kujiokoa.

"Katika kuzilinda njia hizo serikali imeamua kuwashirikisha wananchi na kujaribu kuchambua matumizi bora ya ardhi ili kulinda maisha ya wananchi na mali zao, lakini wanyamapori kulindwa na kuhifadhiwa," alisema mtaalamu huyo. Naye Mkurugenzi wa utafiti Tume ya Taifa ya Mipango na Matumizi ya Ardhi, Dk. Joseph Layson (NLUPC), alisema ukanda wa wanyamapori ni maeneo ambayo hufanya eneo salama la mpito kwa wanyama wanaohama na wanaweza kuishi na kustawi katika makazi hayo kwa muda usiojulikana. Alisema njia za kihistoria za wahamiaji zinaharibiwa haraka kutokana na mabadiliko ya mifumo ya matumizi ya ardhi na mabadiliko ya hali ya hewa.

Alisema harakati za wanyamapori zimehitimisha changamoto mbalimbali za wanadamu na wanyamapori, ambazo upunguzaji wake hauwezi kuachwa kwa serikali pekee.

Alisema, lazima kuwe na suluhu zenye manufaa kwa wanyamapori na wananchi, kuboresha maisha na uchumi wao, kuwa wazi kwa wamiliki wa ardhi na kuboresha ushirikiano na ushiriki wa umma.

"Ardhi ikitunzwa na kuhifadhiwa husaidia wanyama na vilivyomo kuongezeka, kuondoa migongano kati ya uhifadhi na wakulima, ambapo kazi yetu kubwa ni kulinda rasilimali ya ardhi na kuhifadhi mazingira ikiwamo vianzio vya maji," alisema Dk. Joseph.

Kwa upande wake Mwenyekiti wa JET, Dk. Elen Utaro, alisema chama hicho kitaendelea kuwajengea uwezo waandishi wa habari kwa kutumia taaluma yao katika uhifadhi wa mazingira na wanyamapori.

Alisema, Tanzania bado ipo katika mchakato wa kuhifadhi rasilimali kwa sababu kadri siku zinavyokwenda wanyama wanazidi kupungua na wapo katika hatari ya kupotea kutokana na wananchi kuingia katika maisha ya wanyamapori na ushoroba.

# Mwinyi aziagiza wizara ununuzi wa kimtandao

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

RAIS wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, ameziagiza wizara zote za serikali, kuanza kutumia mfumo wa ununuzi kwa njia ya mtandao (eProcurement).

Dk. Mwinyi aliyasema hayo katika uzinduzi wa mfumo wa ununuzi kwa njia ya mtandao (eProcurement), hafla iliofanyika mjini hapo.

Alisema suala la ununuzi limegubikwa na urasimu na kuna nyakati shughuli za utekelezaji wa mipango serikalini huchelewa au kukwama kwenye vitengo vya ununuzi.

Alisema pamoja na vitengo vya ununuzi kutakiwa kuzingatia misingi ya uadilifu na uwazi, lakini kumekuwapo na baadhi ya watumishi walioridhika na hali iliyopo na kuibua urasimu, jambo linalowavunja moyo wazabuni, wawekezaji na wafanyabiashara wanaotoa huduma serikalini.

Aidha, alibainisha kuwapo baadhi ya viongozi na watendaji wanaojaribu kwa njia za siri kupinga matumizi ya mifumo ya kielektroniki ili kulinda maslahi yao binafsi. "Naagiza kila taasisi yenye jukumu la kufanya manunuzi ihakikishe inatumia mfumo huu katika mwaka wa fedha wa 2022/2023 unaoanza," alisema.

Pia, aliagiza kuchukuliwa hatua kali za kisheria watendaji wa ngazi zote watakaoharibu au kudharau kwa makusudi kutumia mfumo huo. Alisema juhudi za kuunda mifumo zinapaswa kuambatana na utekelezaji wa mikakati imara ya utoaji wa mafunzo kwa watendaji wanaosimamia mfumo hiyo, sambamba na elimu hiyo kutolewa kwa wananchi.

Wazabuni na wafanyabiashara wanahitaji kupewa mafunzo ya msingi na kuelimishwa juu ya umuhimu wa kutumia mfumo huo mpya, sambamba na taasisi zinazosimamia utawala bora, hasa Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uhumi Zanzibar (ZAECA), pamoja na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) kufahamu vyema matumizi ya mifumo inayoundwa.

Alisema mfumo wa ununuzi kwa njia ya mtandao utaondoa urasimu, kuimarisha uwazi, uadilifu pamoja na kuondoa kasoro za uwajibikaji ambazo hutumika kupanua mianya ya rushwa.

Naye Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora, Haroun Ali Suleiman, alisema mfumo huo utaleta mafanikio makubwa na kubainisha azma ya wizara hiyo kuhakikisha hauchezewi.

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango, Saada Mkuya Salum, alisema utekelezji wa mfumo huo hautokuwa jambo la hiyari, akaahidi kuusimamia kikamilifu, huku akibainisha kuwapo uadilifu wa kiwango cha chini katika eneo la ununuzi serikalini.

Alisema wizara hiyo inakamilisha taratibu za kubadili Sheria ya Manunuzi ya Mwaka 2011 ili kuendana na wakati uliopo na kuwataka viongozi serikalini kuwa tayari kwa jambo hilo.

"Hatutopokea manunuzi yoyote baada ya kukamilika kwa mfumo huu kwenda kwenye makaratasi," alisema.

Kwa upande wake Katibu Mkuu Ofisi ya Rais Fedha na Mipango, Dk. Juma Malik Akil, alisema lengo la kuandaa mfumo huo ni kuongeza ufanisi na kuwapo usahihi katika mchakato wa ununuzi serikalini.

Alisema ushirikiano mzuri uliopatikana kutoka sekta mbalimbali umechangia kwa kiasi kikubwa kuandaa mfumo huo, ambao ni bora katika nchi za Afrika Mashariki.

Mkurugenzi Mtendaji wa Oman Data Park, Maqbul Salim Alwaheed, alisema mfumo huo sio tu utaleta ufanisi katika ukusanyaji na matumzii ya fedha za serikali, bali utaweka mazingira bora katika masuala mbalimbali, ikiwamo ajira.

Aidha, Mkurugenzi Mtendaji wa eGovernment, Said Seif, alisema mafanikio ya kuwapo kwa mfumo huo yatategemea taasisi mbalimbali za serikali pamoja na vitengo vya manunuzi watakavyoupokea na kuutumia.

## Mradi wa viungo unavyonufaisha wananchi visiwani

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

SERIKALI ya Zanzibar imesema utekelezaji wa mradi wa viungo unaoendelea visiwani humo unasaidia azma ya serikali katika kuwaletea maendeleo wananchi wake Unguja na Pemba.

Hayo yalisemwa na Waziri wa Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo, Shamata Shaame Khamis, wakati akikabidhi baiskeli 30 zenye thamani ya Sh. milioni 7.5, pamoja na visanduku maalumu vya kuweka na kukopa 80 vyenye thamani ya Shilingi milioni nane katika hafla iliofanyika viwanja vya wizara hiyo Maruhubi, mjini Unguja.

Alisema moja ya azma ya serikali kwa wananchi wake ni kutoa ajira 500,000 na kupitia utekelezaji mradi huo, umesaidia kupunguza kundi kubwa la vijana ambao wanaendelea kusaidiwa na hatimaye kujiajiri wenyewe kupitia sekta ya kilimo.

Alitoa mfano miongoni mwa nafasi za ajira zilizotengenezwa na mradi huo ni pamoja na ujenzi wa soko jipya la viungo linaloweza pia kuhifadhi mboga bila kuharibika lililopo Darajani, Mjini Unguja, kuwa ni kielelezo kuwa mradi huo umekwenda kuwakomboa wengi na kuisaidia serikali kuleta maendeleo. Waziri Shamata aliwataka wasimamizi wa vikundi vya kuweka na kukopa waliopatiwa mafunzo maalumu katika utekelezaji mradi, kuhakikisha wanazitumia vyema baiskeli hizo vijijini mwao na kuongeza chachu ya maendeleo na kuwa sababu ya kuleta mabadiliko.

Naye Meneja Mkuu wa mradi wa viungo, Amina Ussi Khamis, alisema mradi huo unatekelezwa na jumuiya isiyo ya kiserikali (Peoples Development Forum), wenye lengo la kuboresha uzalishaji wa kilimo cha mboga, matunda na viungo, chini ya udhamini wa Jumuiya ya Umoja wa Ulaya (European Union).

Alisema lengo kuu la mradi ni kufungua fursa katika mnyororo wa thamani wa bidhaa za matunda, mboga na viungo ili kuongeza uhakika wa chakula na kipato cha wakulima wadogo wanaojishughulisha na kilimo hicho, uzalishaji wa bidhaa zenye viwango bora na utanuzi wa masoko, pamoja na kukuza uchumi wa kilimo ndani ya visiwa vya Zanzibar.

Akizungumzia chamngamoto zilizoonekana kuvikabili vikundi hivyo, alisema ni ukosefu wa elimu ya taaluma za uongozi, ukosefu wa taaluma za kifedha na mipango endelevu ya biashara, pamoja na ukosefu wa misaada ya rasilimali fedha kwa kuendesha vikundi hivyo. Aidha, alisema mradi huo una mpango wa kusaidia vikundi vya kuweka na kukopa kwa kuwapatia ruzuku za kuwasaidia kujiwekeza katika miradi endelevu na yenye manufaa katika jamii.

# Wanafunzi kupewa vyandarua 200,000

**Na Thobias Mwanakatwe,**

SINGIDA

SERIKALI kupitia Mpango wa Taifa wa Kudhibiti Malaria umepanga kugawa vyandarua 200,000 kwa wanafunzi wote wa shule za msingi katika Mkoa wa Singida.

Hatua hiyo ni utekelezaji wa mkakati wa kuifanya Tanzania iwe huru kwa ugonjwa wa malaria ifikapo mwaka 2030.

Mratibu wa Malaria Mkoa wa Singida, Dk. Abdallah Balla, akizungumza na waandishi wa habari, alisema vyandarua hivyo vitagawiwa kwa wanafunzi wa darasa la kwanza hadi saba wa shule za msingi za serikali na zisizo za serikali.

Alisema kutolewa kwa vyandarua hivyo ni moja ya utekelezaji wa afua za kupambana na ugonjwa wa malaria, kwa Mkoa wa Singida kiwango cha maambukizi kimekuwa kikishuka kufikia asilimia 2.3.

Dk. Balla alisema ugawaji wa vyandarua utaanza Julai Mosi, mwaka huu baada ya Bohari Kuu ya Dawa Tanzania (MSD) kuvitoa.

"Serikali imeamua kuwapatia wanafunzi vyandarua kwasababu anakuwa na umiliki na uhitaji kwa hiyo watakwenda kuwa mabalozi wema na hivyo kuongeza matumizi ya vyandarua kwenye jamii," alisema.

Dk. Balla alisema vyandarua hivyo vitagawiwa bila kujali wapo wangapi kwenye kaya kwa kuwa lengo la serikali ni kutaka kuifanya Tanzania iwe huru kwa ugonjwa wa malaria ifikapo 2030.

Vile vile, ili kuhakikisha ugawaji wa vyandarua hivyo unafanikiwa viongozi wa dini wamepewa semina iwasaidie kuwaelimisha wananchi kwenye nyumba za ibada umuhimu wa kuwa na vyandarua.

"Wakati zoezi hili linakwenda kufanyika tunawaomba wananchi kutambua umuhimu wa kulala kwenye chandarua chenye dawa kwani dawa kazi yake ni kupunguza au kuua mbu wanaoneza malaria kwa jamii," alisema, Dk. Balla.

Aliwataka wananchi kuendelea kutunza mazingira kwa kuondoa maeneo ambayo maji yanaweza kutuwama kwa kuwa yanakuwa chanzo cha mazalia ya mbu.

Mratibu wa Kamati ya Viongozi wa Dini, Mkoa wa Singida, Happy Francis, alisema vyandarua hivyo vimekuja katika muda mwafaka, wanafunzi watakapopewa wazazi wahakikishe wanavitumia kwa malengo yanayokusudiwa na sio vinginevyo.

Mwenyekiti wa Kamati za Dini, Mkoa wa Singida, Khamis Kisuke, aliipongeza serikali kwa uamuzi wa kutoa vyandarua hivyo na kuahidi kuwa watahakikisha wanawahamasisha wananchi ili wavitumie kwa lengo la kupunguza zaidi maambukizi ya malaria.

Mchungaji wa Kanisa la Sabato Wilaya ya Manyoni, Joel Ndegea, alisema wananchi wanapaswa kutambua kuwa serikali imetumia fedha nyingi kununua vyandarua hivyo, wahakikishe wanavitumia kupambana na malaria na sio kwenda kuvitumia kuvulia samaki au kufugia kuku.



Ofisa Kilimo wa kampuni ya Bens Agrostar, Frank Miti, akionyesha kiuatilifu cha dawa ya Indozole kwa wakulima.
**PICHA: HAMISI NASRI**

# Mbunge asaidia jimbo lake mafunzo matumizi sahihi viuatilifu, mabomba

**Na Hamisi Nasri,** MASASI

KATIKA kuhakikisha wakulima wa zao la korosho mkoani Mtwara wanakuwa na elimu sahihi ya matumizi bora ya viuatilifu na mabomba wakati wa maandalizi ya mashamba yao, Mbunge wa Jimbo la Ndanda, Cecil Mwambe, kwa kushirikiana na kampuni ya Bens Agrostar pamoja Taasisi ya Utafiti wa kilimo Tanzania (TARI) wameendesha mafunzo maalumu ya matumzi bora ya viuatilifu kwa viongozi wote wa ngazi ya kata wa jimbo hilo.

Mafunzo hayo ya siku moja yaliyofadhiliwa na kampuni ya Bens Agrostar ya jijijini Dar es Saalam, yalifanyika jana mjini Masasi na wadau mbalimbali wa tasnia ya zao la korosho walihudhuria ikiwamo Bodi ya Korosho Tanzania (CBT).

Mbunge huyo alisema, lengo la mafunzo hayo ni kuchochea uzalishaji wa zao la korosho kwa wakulima na kuwafanya wakulima waweze kuwa na uchumi mkubwa ndani ya familia zao.

"Jambo kubwa la msingi leo limefundishwa na wakulima walikuwa hawalifahamu ni kwamba kumbe robo kilo ya salfa ndiyo inapaswa kutumika katika mkorosho ule wenye umri wa miaka kuanzia 20 hadi 30 jambo jingine ambalo limefundishwa ni kwamba sio la mkulima atumie dawa nyingi sana hadi mkorosho wake majani yabadilike rangi kuwa ya njano ndiyo aamini dawa imetosha hapana," alisema Mwambe.

Alisema ofisi yake imeamua kuratibu mafunzo hayo kwa kuwatafuta wataalamu kutoa elimu hiyo ndani ya jimbo lake baada ya kufanya utafiti wa kutosha na kubaini changamoto kubwa iliyoko kwa sasa kwa wakulima wa zao la korosho nchini ni matumizi sahihi ya viuatilifu na kupitia elimu hiyo itawasaidia.

Alisema, ili mkulima afanikiwe kupata mazao ya kutoka ni lazima kuwa na uwelewa wa kutosha wa matumizi bora ya viuatilifu na mabomba ili anapofanya kilimo cha korosho afahamu hatua zote za upuliziaji wa mikorosho yake.

Akitoa mafunzo hayo kwa viongozi hao wa kata kutoka Jimbo la Ndanda, Mtafiti kutoka Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania (TARI), Naliendele Mtwara, Abunueli Boniface, alisema taasisi hiyo imetoa mada kuu tatu kwenye mafunzo hayo ikiwamo jinsi ya kutambua magonjwa mbalimbali yanayoathiri miti ya mikorosho pamoja na wadudu waharibifu na namna ya kupambana nao.

Alisema TARI imefundisha njia mbalimbali za kutatua changamoto hizo kwa wakulima katika matumizi bora ya viuatilifu ikiwamo njia za kisasa na za kienyeji lengo likiwa kila mkulima awe na elimu sahihi ya kupambana na magonjwa yanayoathiri miti ya mikorosho hatimaye aweze kuongeza tija katika zao hilo.

Ofisa kilimo kutoka kampuni ya Bens Agrostar, Frank Miti, alisema licha ya kampuni hiyo kuuza na kusambaza viuatilifu, pia wanatoa elimu kwa wakulima ya namna bora ya matumizi sahihi ya viuatilifu na hadi sasa wamewafikia wakulima wengi zaidi katika mikoa ya Kusini wanakolima korosho.

"Kampuni ya Bens Agrostar imebaini kuwa wakulima wengi wamekosa elimu sahihi ya kutumia mashine ya kupulizia kuanzia jinsi ya kuwasha, namna bora ya uchanganyaji wa dawa na kuzitia ndani ya mashine," alisema Miti.

Kwa upande wao washiriki wakiwamo madiwani, maofisa kilimo, maofisa uvuvi na kilimo, wamempongeza mbunge huyo kwa kuwafanikisha utoaji mafunzo hayo na kwamba yamewaongezea mambo mengi ya msingi ambayo awali walikuwa hawayafahamu.

## Mabinti 52 mazingira magumu wafundishwa ufundi ushonaji

**Na Francis Godwin,** IRINGA

MABINTI 52 toka mazingira magumu ambao baadhi yao walikatisha masomo kutokana na kupata ujauzito wakiwa shuleni katika Wilaya ya Mufindi, mkoani Iringa wameanza kupatiwa mafunzo ya ufundi wa kushona ili kupunguza adha ya ugumu wa maisha kwa kukosa ajira.

Wakizungumza jana wakati wa mafunzo hayo yanayoendelea Mufindi, wamesema mafunzo hayo ni ukombozi kwao.

Elikana Mduvike, Mgede Chang'a na Rebecca Kigulu, washiriki wa mafunzo hayo walisema kabla ya mafunzo hayo hawakuwa na ndoto nyingine ya kuendesha maisha yao.

Walisema wao ni baadhi ya mabinti waliokatishwa ndoto ya maisha kutokana na mimba za utotoni na kupitia mafunzo hayo wana uhakika wa kufanya maisha yao yawe mazuri zaidi.

Aidha, Halmashauri ya Wilaya ya Mufindi, mkoani Iringa kwa kushirikiana na mradi wa Youth Agency Mufindi (YAM), umeanza kutoa mafunzo ya kutengeneza pikipiki kwa vijana 48 kutoka kwenye mazingira magumu.

Mkufunzi wa mafunzo hayo, Longinus Ngonyani, alisema kumekuwapo na mafanikio ya mafunzo hayo toka alipoanza kuwa na washiriki hao baada ya kuanza kuonyesha mwanga wa kuwa mafundi.

Meneja wa mradi wa YAM, Zilipa Mgeni, alisema mradi huo unatekelezwa na Halmashauri ya Mufindi chini ya mradi wa Foxes Community and Wildlife Conservation (FCWC) na YAM kupitia ufadhili wa Finland utatekelezwa kwenye kata za Luhunga, Ihanu na Mdabulo na utanufaisha vijana na watoto wanaotoka katika familia duni zaidi ya vijana 770 katika vijiji 16.

HABARI KIMATAIFA

## Biden asisitiza umoja kwa mataifa ya G7

**NEW YORK,** Marekani

RAIS wa Marekani, Joe Biden, amepongeza muungano wa kimataifa katika kukabiliana na Russia.

Pongezi hizo alizitoa katika kipindi ambacho yeye na viongozi wengine wa mataifa yaliyopiga hatua kiviwanda G7 wakiweka mikakati kuendeleza shinikizo katika jitihada zao za kuitenga Russia.

Katika mkutano wa utangulizi, kabla ya ule wa kilele wa G7 wa jimboni Bavaria, Biden akiwa na mwenyeji wake Kansela wa Ujerumani Olaf Scholz, ambaye ni mwenyekiti wa sasa wa ushirikiano wa mataifa hayo, alisema lazima kuwe na hakikisho la kuendelea kuwa wamoja.

Kiongozi huyo wa Marekani aliongeza kwamba wataendelea kuzifanyia kazi changamoto za kiuchumi, kukabiliana nazo na kuzishinda.

Biden na viongozi wenzake wanakutana kwa siku tatu kwa lengo la kujadili jinsi ya kupata uhakika wa nishati na kukabiliana na mfumuko wa bei, kwa lengo la kuzuia kuporomoka kwa uchumi kwa jitihada yao ya kuiadhibu Russia.

**RUSSIA INATUMIA NJAA SILAHA YA KIVITA**

Rais wa Baraza la Ulaya, Charles Michel amekilaani kitendo cha Russia kutumia njaa kama silaha ya kivita akisema, serikali ya taifa hilo inawajibika kwa shida ya chakula duniani na mateso kwa mataifa masikini.

Akizungumza kabla ya kuanza kwa mkutano wa kilele wa viongozi wa mataifa saba yaliyopiga hatua kiviwanda ya G7m katika jimbo la Bavaria, kusini mwa Ujerumani, Michel alisema serikali ya Russia inatumia chakula kama silaha ya kivita isiyo na sauti.




Kifaru cha Russia kikiwa katika mji wa Severodonetsk baada ya kupata udhibiti kamili jana. **PICHA: DW**

KINACHOENDELEA UKRAINE

# Russia yapeleka nyuklia Belarus

• Yauteka Severodonetsk, yasonga mbele

**KYIV,** Ukraine

RAIS wa Russia, Vladimir Putin, ameahidi kupeleka nchini Belarus, mifumo ya Iskander-M ambayo ina uwezo wa kufyatua makombora ya nyuklia.

Hatua hiyo imekuja wakati vikosi vya Russia vimechukua udhibiti kamili wa mji wa Sieverodonetsk.

Russia inanuia kupeleka mifumo hiyo katika miezi michache ijayo.

Rais Vladimir alisema hayo jana kupitia televisheni ya nchi hiyo wakati wa kuanza kwa mkutano kati yake na kiongozi wa Belarus Alexander Lukashenko mjini Saint Petersburg.

Putin alisema nchi yake itaisaidia Belarus kuboresha ndege zake za kivita aina ya Su-25 kuziwezesha kubeba silaha za nyuklia.

Rais wa Belarus Lukashenko alielezea wasiwasi wake kuhusu kile alichokiita uchokozi na sera za kuudhi za majirani zake Lithuania na Poland.

Alimwomba Putin kuisaidia kuwa na 'majibu yanayofanana' na kile alichosema kuwa ndege za kivita za nyuklia zinazoongozwa na Jumuiya ya Kujihami ya NATO, kuruka karibu na mpaka wake.

Putin alisema haoni sababu ya kuwa na majibu yanayofanana lakini ndege za kivita za Belarus zilizotengenezwa Russia chapa Su-25 zinaweza kuimarishwa zaidi kukihitajika kwenye viwanda vya ndani ya nchi yake.

Mfumo wa makombora Iskander-M ambao NATO huuita SS-26, ulichukua mahala pa Scud, huweza kufyatua kombora umbali wa kilomita 500 na huweza kubeba zana za vita au vichwa vya nyuklia.

**Meya wa mji huo, Oleksandr Stryuk, alisema kwenye runinga ya kitaifa kuwa sasa wanajaribu kuweka utaratibu wao wenyewe kusimamia mji huo, wanachojua tayari wameshaweka kamandi ya aina fulani.**

**RUSSIA YACHUKUA UDHIBITI SIEVERODONETSK**

Vikosi vya Russia vimechukua udhibiti kamili wa mji wa Sieverodonetsk ulioko mashariki mwa Ukraine.

Pande zote mbili zimethibitisha hayo, ikiwa ni pigo kubwa kwa Ukraine kwenye mapambano makali ya zaidi ya mwezi mmoja kuupigania mji huo wa kimkakati.

Hatua hiyo inabadilisha uwanja wa mapambano mashariki mwa Ukraine baada ya wiki kadhaa uwezo wa kijeshi wa Urusi ulileta matokeo kidogo.

Ukraine imesema kuondoka kwao katika mji huo ni hatua ya kimkakati ili kupigana wakiwa eneo ambalo limeinuka mjini Lysychansk ulioko ukingo wa upande mwingine wa mto Siverskyi Donets.

Russia ilisema inalenga kusonga mbele kukamata maeneo zaidi katika ukingo ulioko mkabala, huku Ukraine ikitumai maafa ambayo Russia ilipata katika mapambano ya kukamata SIeverodonetsk, yamevidhoofisha vikosi vyake na kuviweka katika hatari ya kushambuliwa.

Wakati hayo yakijiri waasi wanaotaka kujitenga na Ukraine na wanaounga mkono Russia walisema vikosi sasa vinashambulia mji wa Lysychansk.

**ZELENSKY AAHIDI KUREJESHA MIJI**

Rais wa Ukraine, Volodymyr Zelensky, aliapa kuurudisha mji uliochukuliwa mikononi mwao ukiwamo mji wa Sieverodonetsk.

Kwenye hotuba yake kwa njia ya video, Zelensky amekiri kuwa maafa yanayotokana na vita hivyo kuwa pigo la kihisia.

"Hatujui vita vitadumu kwa muda gani, wala mapigo mangapi tutapata, juhudi zitahitajika kabla ya ushindi kupatikana." Alisema.

Aliongeza: "Mji sasa upo chini ya udhibiti kamili wa Russia,"

Meya wa mji huo, Oleksandr Stryuk, alisema kwenye runinga ya kitaifa kuwa sasa wanajaribu kuweka utaratibu wao wenyewe kusimamia mji huo, wanachojua tayari wameshaweka kamandi ya aina fulani.

Kyrylo Budanov, mkuu wa idara ya intelijensia ya Ukraine aliliambia shirika la habari la Reuters kwamba Ukraine inachukua hatua ya kimkakati ambayo ni kujikusanya na kuviondoa vikosi vyake Sieverodonetsk.

"Urusi inatumia mbinu iliyotumia Mariupol, kuuharibu mji kabisa," alisema.

Alisema kutokana na hali hiyo wamapambana kwenye mahame yaliyoharibiwa ya mji huo hakuwezekani tena.

Alisisitiza vikosi vya Ukraine vinaondoka kuelekea maeneo ya juu ili kuendelea na operesheni yao ya ulinzi.

**PUTIN KUFANYA ZIARA YA NJE YA URUSI**

Rais Vladimir Putin, anatarajiwa kuyatembelea mataifa mawili madogo ya eneo la Kati la Asia ya uliokuwa Umoja wa Kisovieti wiki hii.

Ziara hiyo inatafsiriwa inaweza ya kwanza ya kiongozi huyo wa Russia kutoka nje ya mipaka ya taifa lake tangu alipoamuru uvamizi wa Ukraine.

Televisheni ya nchi hiyo ilisema Putin atayatembelea mataifa ya Tajikistan na Turkmenistan na baadaye atarejea nyumbani kukutana na Rais wa Indoneshia Joko Widodo.

Safari ya mwisho ya Putin nje ya nchi yake ilikuwa ya nchini China mapema Februari, ambapo yeye na Rais wa China Xi Jinping walizindua mkataba wa urafiki usio na ukomo, muda mfupi kabla ya wote wawili kuhudhuria sherehe za ufunguzi wa michezo ya Olimpiki ya majira ya baridi. **DW**

HABARI MICHEZO

# MBEYA KWANZA YA KWANZA KUSHUKA

Na Adam Fungamwango

KIPIGO cha mabao 2-1 ilichokipata juzi kwenye Uwanja wa Majimaji Songea dhidi ya Ruvu Shooting, kimeifanya timu ya Mbeya Kwanza kuwa ya kwanza kushuka daraja kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara msimu huu.

Timu hiyo kutoka Mbeya, iliyokuwa ikitumia uwanja huo ulio mkoani Ruvuma, imeaga rasmi Ligi Kuu baada ya kupanda msimu huu na kuendeleza rekodi ya kushuka kwa angalau timu moja inayopanda daraja kila msimu.

**Kwa msimu kadhaa sasa timu zinazopada Ligi Kuu, moja ni lazima itashuka msimu huo huo, kama ilivyokuwa kwa Ihefu msimu uliopita ambayo nayo imerejea tena kwa msimu ujao.**

Ni mabao ya Rashid Juma na Fullzulu Maganga yaliyoizamisha Mbeya Kwanza, huku Oscar Mwajanga akifunga la kufutia machozi.

Mbeya Kwanza imeshuka baada ya juzi hiyo hiyo, Biashara United kuifunga KMC bao 1-0, na kufikisha pointi 28, ambazo haiwezi kuzifikia.

Timu hiyo yenye pointi 24 na kuendelea kushika mkia, hata ikishinda mechi yake moja iliyobaki, itafikisha pointi 27, ambazo zimeshapitwa na Bishara United, hivyo itamaliza ligi kwenye nafasi ya 15, ambayo pamoja itakayoshika nafasi ya mwisho ya 16, zote zinatakiwa kushuka moja kwa moja.



Rais wa Shirikisho la Soka TFF, Wallace Karia (kulia), akizungumza jambo na viongozi mbalimbali akiwapo Mwenyekiti wa Bodi ya Ligi, Steven Mnguto (kushoto), Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera, Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Innocent Bashungwa na Mkurugenzi Mkuu wa NBC, Theobald Sabi, katika hafla ya kukabidhi Kombe kwa Mabingwa wa Ligi Kuu ya NBC, Yanga kwenye Uwanja wa Sokoine, Mbeya juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# *Bondia Chokoraa amtwanga Mpango*

Na Saada Akida

MABONDIA Khareed Chokoraa na msanii wa bendi ya African Stars, Twanga Pepeta usiku wa kuamkia jana Jumapili amefanikiwa kumchapa mpinzani wake Juma Mpango kwa KO, huku Emmanuel Mwakyembe akimpiga Hamisi Morinyo kwa TKO na kumaliza utata wa Mburahati na Manzese.

Chokoraa alishinda kwa KO ya raundi pili katika pambano hilo usiku wa Kisasi wakati Mwakwenye akimchapa Morinyo kwa TKO ya raundi ya sita.

Morinyo kutoka Mburahati na Mwakyembe wa Manzese ambao walicheza pambano kuu kwa raundi nane, lakini liliishia raundi ya sita kwa TKO baada ya mwamuzi kumaliza kwa kumuokoa Morinyo ambaye alikuwa amechapika vilivyo.

Licha ya Morinyo kuonyesha usugu na uvumilivu, lakini haikuweza kumsaidia kutokana na kupigwa ngumi nyingi ambazo ziliweza kumlewesha kabla ya kwenda chini na mwamuzi kumaliza pambano.

Baada ya pambano hilo, Morinyo amekiambia Kijiwe cha Ndondi kwa kudai kuwa amepigana katika pambano hilo lakini hakuwa sawa kiafya kutokana na kusumbuliwa na tatizo la macho hivyo imepelekea yeye kupoteza pambano hilo.

Kwa upande wa Mwakyembe alisema kuwa ushindi katika pambano hilo kwake ulikuwa wa lazima kwa kuwa alijiandaa kumchapa mpinzani wake.



## Wasanii wafanya kweli tamasha la Zege Day

Na Sabato Kasika

MSANII mkongwe wa muziki wa kizazi kipya, Chege Chigunda au 'Mtoto wa Mama Said', ni mmoja wa wasanii waliotia fora kwenye tamasha la Zege Day lililofanyika juzi kwenye viwanja vya Mwembeyanga Temeke Dar es Salaam.

Akiwa na wacheza shoo wanne wa kike, Chege aliimba wimbo wake wa miaka mingi wa 'Nyumbani ni nyumbani' akipokezana na mashabiki waliokuwa kwenye viwanja hivyo, huku akishangiliwa kwa nguvu.

Naye MC Kinata, anayeimba singeli aliamsha shangwe hata waliokuwa mbali wakasogea karibu kuimba wimbo wake wa 'Si unajua singeli inavyobamba uswahili' na kufuatiwa na msanii mwingine Moni Centrozone.

Kwa upande wake Nedy Music alitoa burudani akifuatiwa na Lody Melody, ambapo baadaye Jose Mara akiwa na bendi yake ya Mapacha Music akapanda jukwaani kufanya vitu vyake.

Alipiga muziki wa dansi iliochanganyika na Bongo Fleva, kisha wasanii wengine akiwamo Kicheko, Kayumba na Mzee wa Bwax nao kila mmoja akapa jukwaani kwa nafasi yake kufanikisha tamasha hilo.

## Arusha yasubiri kwa hamu fainali FA

**Na Cheji Bakari,** TANGA

CHAMA cha Soka Mkoa wa Arusha, (ARFA) kimesema kuwa usalama upo imara mkoani humo kuelekea fainali ya Kombe la Shirikisho (FA) kati ya Yanga na Coastal Union itakayopigwa Julai 2 mwaka huu, kwenye Uwanja wa Sheikh Amri Abeid.

Mwenyekiti wa chama hicho, Zakayo Mjema ameliambia Nipashe kwa njia ya simu kuwa kuelekea fainali hizo, maandalizi yote muhimu yameshakamilika kwa zaidi ya asilimia 90 ikiwamo suala la ulinzi na usalama.

Amesema: "Arusha tuna uzoefu wa mechi kubwa, kuhusu suala la ulinzi na usalama upo imara kwa timu na washabiki watakaokuja kushuhudia mechi hiyo, watakuja na wataondoka salama."

Aliongeza:" Serikali ya mkoa wa Arusha, serikali ya wilaya, ARFA pamoja na Jeshi la Polisi wamefanya maandalizi ya kutosha kuhakikisha mechi inachezwa eneo salama".

Naye Meneja wa Uwanja wa Sheikh Amri Abeid, Abdallah Kajembe amesema kuwa uwanja upo vizuri na umeshafanyiwa marekebisho katika maeneo yote muhimu ikiwamo eneo la kuchezea, vyoo na majukwaa.

"Sehemu kubwa ya uwanja imeshafanyiwa marekebisho na tunaendelea kufanya marekebisho ya mwisho," alisema.

# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### RONALDO AJADILIWA

MSHAMBULIAJI wa Manchester United na Ureno, Cristiano Ronaldo mwenye umri wa miaka 37, ilikuwa mojawapo ya mada zilizojadiliwa wakati mmiliki mpya wa Chelsea, Todd Boehly alipokutana na wakala wa mchezaji huyo, Jorge Mendes wiki iliyopita. ***(The Athletics)***

### ROMA YAMTAKA RONALDO

AS Roma inataka kumsajili Cristiano Ronaldo na kumuunganisha na bosi wake wa zamani katika klabu ya Real Madrid, Jose Mourinho. ***(Retesport)***

### WERNER KUBADILISHWA

CHELSEA huenda ikamwongeza mshambuliaji wao wa Ujerumani, Timo Werner mwenye umri wa miaka 26, katika mkataba wa kubadilishana na mlinzi wa Juventus na Uholanzi, Matthijs de Ligt mwenye miaka 22. ***(Sky Sports)***

### DE JONG NA MAN

KLABU ya Manchester United inazidi kuwa na uhakika wa kumpata mchezaji Frenkie de Jong, huku ada ya maafikiano ya takriban pauni milioni 69 ikiafikiwa na Barcelona ili kumnunua kiungo huyo wa kati wa Uholanzi mwenye umri wa miaka 25 ***(Goal).***

### OTAVIO KUUZWA

KLABU ya Porto FC inatarajiwa kuimarisha nia yao ya kumnunua winga wa Ureno, Otavio mwenye umri wa miaka 27 wiki hii baada ya kukataa ofa ya pauni milioni 26 kutoka Leeds United. ***(Mirror)***

### RAPHINHA ANUKIA ARSENAL

ARSENAL inatazamiwa kuongeza juhudi zake za kumsajili mshambuliaji wa Leeds United na Brazil, Raphinha mwenye umri wa miaka 25. ***(The Athletic)***

### NEYMAR AWANIWA

JUVENTUS na Paris St-Germain zimeanzisha mazungumzo yanayohusu kumnunua mshambuliaji wa Brazil, Neymar mwenye umri wa miaka 30, ambaye anahusishwa na Chelsea. (***AS***)

### STERLING ATAKIWA CHELSEA

KOCHA wa Chelsea, Thomas Tuchel amewasiliana na mshambuliaji wa Manchester City, Raheem Sterling mwenye umri wa miaka 27 ili kumsajili.***(Telegraph)***

### WILLIAMS AWINDWA

KLABU ya Nottingham Forest inakaribia kufikia makubaliano ya kumnunua beki wa kulia wa Liverpool, Neco Williams mwenye umri wa miaka 21, ambaye thamani yake ni pauni milioni 15. ***(Sun)***

### WINKS ANUKIA EVERTON

EVERTON na Tottenham Hotspur zinaendelea na mazungumzo yao kuhusu uhamisho wa kiungo wa kati wa Spurs, Harry Winks mwenye umri wa miaka 26. ***(Sky Sports).***

### EBIOWEI ALIIKATAA MAN

WINGA wa England, Malcolm Ebiowei mwenye umri wa miaka 18, alikataa nafasi ya kujiunga na Manchester United akipendelea kuhamia Crystal Palace kwa uhamisho huru kutoka Derby. ***(Sun)***

## DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# GARETH BALE ATUA LIGI KUU MAREKANI

●●● Akubali kujiunga na klabu ambayo mlinzi wa Italia, Chiellini ametua hapo...

**LONDON,** England

GARETH Bale amekubali kuhamia Klabu ya Ligi Kuu ya soka ya Marekani, MLS, LAFC kwa mujibu wa 90min.

**Mchezaji huyo wa kimataifa wa Wales aliondoka Real Madrid mwanzoni mwa msimu huu wa joto na alikuwa akihusishwa na klabu kadhaa zilizoonyesha nia ya kumtaka.**

Bale alikuwa akitafuta klabu mpya ya kucheza soka mara kwa mara katika maandalizi ya kuelekea Kombe la Dunia nchini Qatar baadaye mwaka huu.

Cardiff City ilifanya mazungumzo na Bale juu ya kurejea Wales, lakini vyanzo sasa vimethibitisha kwamba, mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 32 amekubali kuhamia katika Klabu ya LAFC inayoshiriki Ligi Kuu ya MLS.

Kwa mujibu wa 90min, Bale amepewa mkataba wa miezi 12, huku kukiwa na chaguo la kuongezwa miezi 18 hadi mwisho wa msimu wa mwaka 2024 wa MLS.

LAFC tayari ilishamsajili mlinzi wa kati wa Italia, Giorgio Chiellini, ambaye anajiunga kwa uhamisho huru baada ya kumaliza kipindi chake cha miaka 17 kucheza pale Juventus. Chiellini atatambulishwa rasmi Julai 7, wakati dirisha la uhamisho litakapofunguliwa, na Bale atakuwa miongoni mwao.

Wachezaji wote wawili wanatarajia kucheza mechi yao ya kwanza ya LAFC dhidi ya LA Galaxy Julai 8, mwaka huu.

LIVE IN PLAY
CHEZA USHINDE JACKPOT TZS. 267,

MECHI KALI
TREATY UNITED
VERSUS
CORK CITY
1 | 5.10
X | 3.87
2 | 1.55

PIGA *150*87#
Karibu SportPesa
1. Bet Sasa
2. Michezo zaidi
3. JACKPOT
4. Weka Pesa
5. Akaunti yangu
6. Toa Pesa
7. Matokeo ya Bet/Mechi
00. Toka

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, TUPIGIE:
18+ 0764115588, 0677115588
0685115588 GBT:0249
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# DI MARIA ATAKIWA JUVENTUS




**PARIS,** Argentina

ANGEL Di Maria ameisifia Juventus kuwa "klabu kubwa zaidi nchini Italia" wakati akitafakari ofa aliyopewa ya kujiunga na Bianconeri hao.

Di Maria anaondoka Paris Saint-Germain baada ya mkataba wake kufika mwisho, hivyo kumaliza kipindi chake cha misimu saba katika mji mkuu huo wa Ufaransa.

Barcelona na Juventus zote zimeonyesha nia ya kutaka kumsajili mchezaji huyo wa kimataifa wa Argentina, na wiki iliyopita Di Maria alizungumza na ESPN kuhusu ofa aliyopokea.

"Juve ni klabu kubwa zaidi nchini Italia na mojawapo ya timu zinazonivutia. Kwa sasa ninatafakari, " alisema akinukuliwa na ESPN.

Wakati Di Maria akiendelea kuwaniwa na vigogo wawili wa soka la Ulaya, alisisitiza mwezi uliopita kwamba, alitaka kubaki PSG, lakini klabu ilimlazimisha kuondoka.

"(Ulikuwa) uamuzi wa klabu. Kila mtu alijua nilitaka kubaki mwaka mmoja zaidi. Nilitaka kuendelea ili nishinde taji la Ligi ya Mabingwa Ulaya, tulikaribia, hicho ndicho kitu pekee nilichokikosa," aliiambia ESPN, Mei mwaka huu.

"Lakini najua kwamba, vijana wataendelea kwa njia ile ile, watajaribu kushinda. Naitakia mema timu hii, lazima niheshimu uamuzi wa klabu."



# Chelsea kumuuza Ziyech

**LONDON,** England

CHELSEA wamemwambia winga, Hakim Ziyech kwamba, yuko huru kuondoka katika klabu hiyo msimu huu wa joto, huku AC Milan ikiwa miongoni mwa timu zinazotaka kumsajili, kwa mujibu wa Daily Mail.

Ziyech alihamia Stamford Bridge msimu wa joto wa mwaka 2020 kwa ada ya takriban pauni milioni 33, lakini ameshindwa kuwa kwenye kiwango bora kama alichokionyesha katika kipindi chake kizuri akiwa na Ajax, akifanikiwa kufunga mabao 14 na kutoa pasi za mabao kumi katika mechi 83 tangu alipowasili.

Kocha Thomas Tuchel na mmiliki, Todd Boehly wanatafuta wachezaji kadhaa wa safu ya ushambuliaji msimu huu wa joto, huku Ousmane Dembele, Raheem Sterling na Richarlison wakiwa miongoni mwa wanaojadiliwa, na Chelsea pia wamefanya mazungumzo na wawakilishi wa winga wa Ajax, Antony.

Chelsea tayari wamekubali kumtoa kwa mkopo Romelu Lukaku kurudi Inter na vyanzo vimethibitisha kwamba, The Blues hao wako tayari kuachana na Ziyech naTimo Werner na Christian Pulisic.

## HABARI MICHEZO

,714,020

JACKPOT
MECHI WIKI HII

BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE 13

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 28/06/22 | 20:00 | Ghazl EL Mahallah vs Ismaily SC | 3.11 | 2.76 | 2.56 |
| 02. 28/06/22 | 20:00 | Arab Contractors vs National Bank | 2.66 | 2.96 | 2.76 |
| 03. 29/06/22 | 01:00 | Brusque SC vs Bahia BA | 2.79 | 2.94 | 2.50 |
| 04. 29/06/22 | 03:30 | Corinthians vs Boca Juniors | 2.17 | 2.95 | 3.34 |
| 05. 29/06/22 | 13:00 | Daegu vs Pohang Steelers | 2.38 | 3.24 | 2.70 |
| 06. 30/06/22 | 01:00 | Nautico PE vs Criciuma SC | 2.47 | 3.12 | 2.67 |
| 07. 30/06/22 | 01:15 | Talleres vs Colon Santa Fe | 2.26 | 2.95 | 3.14 |
| 08. 30/06/22 | 02:00 | Orlando City vs Nashville SC | 2.32 | 3.15 | 2.85 |
| 09. 30/06/22 | 02:30 | Toronto FC vs Columbus Crew | 2.61 | 3.68 | 2.47 |
| 10. 30/06/22 | 03:00 | Chicago Fire vs Philadelphia Union | 2.47 | 3.27 | 2.86 |
| 11. 30/06/22 | 03:05 | Tlaxcala FC vs Cimarrones De Sonora | 2.41 | 3.10 | 2.76 |
| 12. 30/06/22 | 03:30 | CRB AL vs Tombense MG | 2.27 | 2.94 | 3.13 |
| 13. 30/06/22 | 03:30 | Novorizontino SP vs Vasco da Gama | 2.85 | 2.85 | 2.51 |

MECHI ZA USHINDI

"1" - NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA
"X" - NI TIMU KUTOKA SARE
"2" - NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

JUMATATU - 27/06/2022

| MUDA | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 12:00 | 2353 | Visakha FC vs Bali Utd Pusam | 6.27 | 4.22 | 1.42 |
| 13:00 | 4196 | Phnom Penh vs CLB Viettel | 5.70 | 4.22 | 1.45 |
| 13:00 | 4321 | Fasil Kenema vs Ethiopia Bunna SC | 1.59 | 3.45 | 5.53 |
| 13:00 | 4655 | Mohammedan Sporting Club Dhaka vs Sheikh Jamal | 2.74 | 3.33 | 2.30 |
| 16:00 | 2348 | Arba Minch Kenema vs Saint George FC | 4.50 | 2.94 | 1.86 |
| 16:00 | 5800 | Kedah vs Kaya FC | 1.78 | 3.47 | 4.01 |
| 17:00 | 5058 | Young Elephants FC vs Hougang United | 12.75 | 7.85 | 1.12 |
| 18:00 | 1893 | FK Liepaja vs SK Super Nova | 1.03 | 10.86 | 29.61 |
| 19:00 | 1187 | Grorud IL vs Brann | 9.84 | 6.30 | 1.19 |
| 19:00 | 1381 | Bryne vs Stjordals-Blink | 1.73 | 3.82 | 3.82 |
| 19:00 | 1947 | FS Metta/Lu vs FK Auda | 4.52 | 3.49 | 1.69 |
| 19:00 | 4868 | Sogndal vs Mjondalen | 1.98 | 3.60 | 3.15 |
| 19:00 | 5498 | Ranheim vs Kfum Oslo | 2.35 | 3.44 | 2.61 |
| 19:00 | 5930 | Aasane Fotball vs Sandnes Ulf | 2.72 | 3.46 | 2.26 |
| 19:30 | 3580 | Volda vs Hodd 2 | 1.55 | 4.73 | 4.14 |
| 20:00 | 1450 | Malmo vs Helsingborg | 1.21 | 5.48 | 10.76 |
| 20:00 | 1743 | Kalmar vs IFK Varnamo | 1.81 | 3.29 | 4.12 |
| 20:00 | 2460 | El Gouna vs Eastern Company SC | 1.99 | 3.22 | 3.82 |
| 20:00 | 2667 | Sirius FK vs IFK Goteborg | 2.69 | 3.18 | 2.41 |
| 20:00 | 3745 | Elfsborg vs Varbergs Bois | 1.32 | 4.72 | 7.68 |
| 20:00 | 3950 | Landskrona Bois vs Orebro SK | 2.95 | 3.35 | 2.37 |
| 20:00 | 4089 | Bjarg vs FK Haugesund 2 | 2.04 | 3.68 | 2.95 |
| 20:00 | 4186 | Falkenbergs vs Angelholms | 1.78 | 3.59 | 3.84 |
| 20:00 | 5842 | Farco FC vs El Ittihad Alexandria | 2.86 | 2.91 | 2.61 |
| 20:00 | 5966 | Brommapojkarna vs Osters IF | 2.33 | 3.42 | 2.96 |
| 20:30 | 5817 | Crusaders Belfast vs St Mirren | 6.40 | 4.60 | 1.42 |
| 21:00 | 1827 | Al Hilal Riyadh vs Al Faisaly (KSA) | 1.35 | 5.04 | 7.66 |
| 21:00 | 2568 | Al Raed Club vs Abha | 1.60 | 4.05 | 5.06 |
| 21:00 | 2824 | Dhamk vs Al Taawon | 4.34 | 3.79 | 1.74 |
| 21:00 | 3126 | AL Tai vs AL Hazm | 1.70 | 3.73 | 4.64 |
| 21:00 | 3732 | AL Faiha vs Al-Ettifaq | 4.95 | 3.69 | 1.68 |
| 21:00 | 4522 | Al Shabab Riyadh vs Al Ahli Jeddah | 3.48 | 3.73 | 1.94 |
| 21:00 | 4761 | Sarmiento Resistencia vs San Martin Formosa | 2.00 | 3.05 | 3.95 |
| 21:00 | 5218 | Al Ittihad Jeddah vs AL Baten | 1.30 | 5.45 | 8.47 |
| 21:00 | 5511 | CA Rentistas vs Albion FC | 2.07 | 3.24 | 3.24 |
| 21:00 | 5625 | Al Nasr Riyadh vs Al Fateh (KSA) | 1.55 | 4.43 | 5.03 |
| 21:30 | 2046 | Sportivo Barracas vs Deportivo Muniz | 2.09 | 2.99 | 3.48 |
| 21:30 | 3713 | Patronato Parana vs Independiente | 2.99 | 2.89 | 2.38 |
| 21:30 | 4930 | Sacachispas FC vs CA Atlanta | 2.95 | 2.76 | 2.51 |
| 21:45 | 2591 | Athlone Town vs Waterford Utd | 7.26 | 5.10 | 1.30 |
| 21:45 | 3233 | Bray Wanderers vs Wexford Youths | 2.55 | 3.24 | 2.50 |
| 21:45 | 3669 | St Patricks vs Shamrock Rovers | 4.12 | 3.29 | 1.81 |
| 21:45 | 4214 | Longford Town vs Galway United | 3.44 | 3.34 | 1.96 |
| 21:45 | 4648 | Treaty United vs Cork City | 5.10 | 3.87 | 1.55 |
| 22:15 | 1189 | Kordrengir vs Afturelding | 2.16 | 3.84 | 2.66 |
| 22:15 | 1578 | Grotta vs Throttur Vogum | 1.49 | 4.44 | 4.93 |
| 22:30 | 3022 | Coca Cola vs Talaea El Gaish | 1.90 | 3.16 | 4.32 |
| 22:45 | 4385 | IA Akranes vs Breidablik | 4.91 | 4.42 | 1.49 |
| 23:00 | 3558 | Univ de Chile vs General Velasquez | 1.17 | 6.50 | 10.83 |
| 23:30 | 4979 | Univ San Martin vs Deportivo Municipal | 2.89 | 3.23 | 2.25 |

CHEZA KWA WAJIBU | KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.



# BARBARA ATAJA MECHI 2

**Na Adam Fungamwango**

OFISA Mtendaji Mkuu wa klabu ya Simba, Barbara Gonzalez, amesema katika maisha yake ya soka hatozisahau mechi mbili za timu yake zilizochezwa kwenye nyakati tofauti, ambazo ni dhidi ya Yanga Kombe la FA, na Jwaneng Galaxy ya Botswana ambayo ni ya Ligi ya Mabingwa Afrika.

**Akizungumza jijini Dar es Salaam, alisema kuwa mechi hizo mbili, moja inamkumbusha uchungu alioupata kwa kupoteza, na moja ndiyo iliyompa heshima kubwa hadi leo hii.**

"Mechi iliyonipa uchungu mkubwa ni ile ya Jwaneng Galaxy, ile mechi ni kama wote sisi sijui tulifunikwa na nini. Hadi mapumziko tulikuwa vizuri tu, lakini kipindi cha pili sijui nini kilitokea, sijui tulifunikwa na nini kichwani, na baada ya kupoteza mechi ile ni kama Simba tulisambaratika hivi, hatukuelewa nini kimetokea, na hadi leo hii tunajiuliza nini? Ukweli iliniumiza sana," alisema Barbara.

Kwenye mechi hiyo iliyochezwa Oktoba 24, 2021, Uwanja wa Benjamin Mkapa, Simba ilichapwa mabao 3-1 na kuondolewa kwenye Ligi ya Mabingwa Afrika, ikaangulia Kombe la Shirikisho na kuishia hatua ya robo fainali.

Aliitaja mechi ya kukumbukwa, aliyoipenda na kumpa heshima kubwa ni ile ya fainali ya Kombe la FA msimu uliopita iliyochezwa kwenye Uwanja wa Lake Tanganyika Kigoma, Simba ikishinda bao 1-0, lililofungwa na Thadeo Lwanga.

"Mechi niliyokuwa na furaha ni ile ya Kigoma dhidi ya Yanga, ile mechi ilikuwa na maana kubwa kwangu, maana wiki nzima nilikuwa nashambuliwa, natukanwa, lakini sikusema chochote, ilikuwa inaniumiza, tulipo-shinda nikashukuru Mungu, alionyesha ukubwa, watu wengi walinilaumu mimi, ni mechi ambayo nimelia, lakini Mungu alitupa furaha na kutwaa Kombe la FA, ikanipa heshima kubwa," alisema.

Ikumbukwe kuwa wiki moja kabla ya mechi hiyo kuchezwa Julai 25, 2021, aliyekuwa Ofisa Habari wa klabu hiyo Haji Manara alikuwa ameondoka kwenye klabu hiyo, huku kukiwa na maneno mengi yakimhusisha ofisa mtendaji huyo, lakini baada ya mechi hiyo, baadhi ya wanachama na mashabiki wa Simba walimpongeza, kumsifu, kisha kuheshimu na kumwamini kwa kila maamuzi anayofanya hadi leo hii.




Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Tulia Ackson (kulia) akifurahi pamoja na Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo wa Zanzibar, Tabia Maulid Mwita, wakati akielekea kupokea medali yake baada ya kuibuka mshindi wa kwanza katika mbio za mita 100, katika Bonanza la Pamoja la Benki ya CRDB (CRDB Bank Pamoja Bonanza), lililofanyika kwenye Uwanja wa Jamhuri, jijini Dodoma Juni 25, 2022. Wengine pichani wakishuhudia ni Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi wa Benki ya CRDB, Dkt. Ally Laay pamoja na Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya CRDB, Abdulmajid Nsekela. **PICHA: MWANDISHI WETU**

# *CRDB Bank Pamoja Bonaza yafana Dodoma*

**Na Mwandishi Wetu**

SPIKA wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dk. Tulia Akson ameipongeza Benki ya CRDB kwa kuendelea kuandaa bonanza la pamoja la michezo lililopewa jina la "CRDB Bank Pamoja Bonanza" kwa mafanikiao makubwa pamoja na kuhamasisha utamaduni wa kushiriki katika michezo na kujenga afya na kuhamasisha mshikamano kwa Watanzania katika shughuli za maendeleo.

Akizungumza katika bonanza hilo juzi, Tulia alisema bonanza hilo limeleta msisimko na mwamko mkubwa kulinganisha na miaka ya nyuma, ambapo mwaka huu idadi ya washiriki imeongezeka na kufanya maana na lengo halisi la mashindano hayo kupata umaarufu jijini Dodoma na Tanzania kwa ujumla.

"Kwa mwaka huu tumeona hata ndugu zetu wa Baraza la Wawakilishi Zanzibar na pia vijana wetu wa Bongo Flava ambao kwa pamoja wameleta msisimko mkubwa na kuleta ushindani, hongereni sana ndungu zetu Bemki ya CRDB kwa kuwa na maono makubwa hivi," alisema Tulia.

Kwa upande wake Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya CRDB, Abdulmajid Nsekela alisema wao wanan-aipa kipaumbele michezo, kwani m ni afya, inaleta umoja na upendo, na pia kuwawaleta pamoja wafanyakazi na wadau mbalimbali wa michezo nchini.

"Benki inatumia bonanza hili kama sehemu tu ya kuisogeza karibu na Serikali, Bunge na wadau mbalimbali nchini ili kupata nafasi ya kusikiliza mahitaji yaliyopo na kujua namna gani benki inaweza kushiriki katika mipango ya maendeleo ya nchi na kuthibitisha kauli mbiu yake ya "Ulipo Tupo" na kuwa ni benki inayomsikiliza mteja," alisema Nsekela.

Naye Mwenyekiti wa Bodi wa CRDB, Ally Laay aliwashukuru Wabunge na wadau mbalimbali wa serikali na wananchi waliohudhuria mashindano hayo na kujitokeza kwa wingi kushiriki bonanza hilo lililotanguliwa na matembezi yaliyo anzia katika viwanja vya bunge vikiwemo vikundi mbalimbali vya Jogging, wanafunzi wa vyuo na Sekondari pamoja na wananchi kwa kutambua umuhimu wa michezo.

# Michezo

Jumatatu Juni 27, 2022

Nipashe




Bale atua Ligi Kuu Marekani UKURASA 21

# Yanga yaiteka Dar

## Mapokezi yake ni kufuru, barabara zafungwa...




Saada Akida na Shufaa Lyimo

ILIKUWA ni majira ya saa 6:00 wakati kikosi cha mabingwa wa Ligi kuu Tanzania Bara, Yanga kilipowasili kwenye Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Julius Nyerere jijini Dar es Salaam wakitokea Mbeya na kombe, huku wakilakiwa na malefu ya mashabiki wao.

**Yanga ambayo ilitua kwa ndege ya Air Tanzania, juzi Jumamosi ilikabidhiwa rasmi kombe la ubingwa huo jijini Mbeya na Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Innocent Bashungwa, baada ya kutoka sare ya kufungana bao 1-1 na Mbeya City.**




Matukio mbalimbali ya mapokezi ya wachezaji na benchi la ufundi la timu ya Yanga wakati walipowasili katika Uwanja wa Kimataifa wa Julius Nyerere, Dar es Salaam jana. **PICHA ZOTE: JUMANNE JUMA**

Yanga baada ya kutua kwenye uwanja wa ndege wachezaji wakiwa na kombe waliingia kwenye basi maalumu ambalo juu lilikuwa wazi ili wachezaji waweze kuonekana na kombe hilo na kuanza safari ya kuelekea makao makuu ya klabu hiyo.

Maelfu ya mashabiki walimiminika barabarani na kusababisha baadhi ya barabara kufungwa ili kupisha msafara huo, huku wakiimba na kucheza kwa furaha kubwa.

Barabara ya Nyerere ilikumbwa na foleni kubwa wakati mashabiki hao wakiendelea kulisindikiza gari la wachezaji hao na wengine wakijaa katika daraja la juu la Mfugale maeneo ya Tazara na kusababisha magari mengine kushindwa kupita kutokana na umati wa mashabiki.

Shangwe zaidi ziliibuka wakati basi hilo lilipokatiza mitaa ya Msimbani kwa wapinzani wao Simba na kufanya shughuli kwenye maeneo hayo kusimama kwa muda na kelele na shangwe nyingi kuibuka.

Wachezaji pamoja na mhamasishaji wao, Haji Manara walishuka na kombe hilo chini jirani na makao makuu ya Simba na kupiga nalo picha huku shangwe zikitawala.

Baada ya hapo walielekea kwenye makao makuu ya klabu, Jangwani ambako walikaa kwa muda kabla ya uongozi kutangaza kwamba, wanakwenda mtaa wa Samora ambako walitarajiwa kuzungumza na mashabiki.

Wakati shangwe hizo zikiendelea, Uongozi wa Yanga umesema bado wana kazi kubwa ya kuendelea kuwapa furaha mashabiki wake kwa kutwaa taji la Kombe la Shirikisho (FA) wakati watakapokutana na Coastal Union Julai 2, mwaka huu, jijini Arusha.

Wakizungumza kwa nyakati tofauti, Kocha Msaidizi wa Yanga, Cedric Kaze alisema kutwaa ubingwa huo ni furaha kwa kila Mwanayanga na bado wanahitaji kuwapa furaha kubwa kwa kupambana na kupata matokeo mazuri katika michezo yao miwili iliyobaki.

Alisema wanaenda kujiandaa vizuri kwa ajili ya kupata matokeo mazuri katika mchezo wao wa Jumatano dhidi ya Mtibwa Sugar ambao utakuwa ni wa mwisho kwenye Ligi na kuelekea katika fainali yao dhidi ya Coastal Union.

"Tumepata ubingwa ni furaha kubwa hasa tulipitia kipindi kigumu sana na sasa wanasubiri kwa hamu kubwa, wachezaji sasa warudi mchezoni kwa sababu bado tuna kazi kubwa mbele katika michezo miwili iliyosalia ikiwamo Ligi dhidi ya Mtibwa Sugar na kombe la Azam na Coastal Union," alisema.

Naye mshambuliaji wa timu hiyo, Heritier Makambo alisema wamefurahi kutwaa ubingwa, lakini bado haijamaliza kazi kwa sababu wanahitaji kutafuta ushindi katika michezo iliyobakia ikiwe kutwaa kombe la FA.

Meneja wa timu hiyo, Hafidhi Saleh alisema kwake ni furaha kwa Yanga kutwaa ubingwa huo tena bila ya kupoteza mechi lakini watazidi kufurahi watakapofanikiwa kutwaa Kombe la Shirikisho.

Alisema baada ya kuhakikisha wanapata mataji hayo yote matatu lakini wanahitaji kuyalinda kwa misimu ijayo kwa viongozi kuweka mikakati imara.

## Simba yateseka kwa Prisons

Na Adam Fungamwango

BAO lililofungwa na Benjamin Asukile dakika ya 52, lilitosha kuiangamiza Simba jana kwenye Uwanja wa Sokoine jijini Mbeya na kuifanya Prisons kujiweka kwenye mazingira mazuri ya kubaki Ligi Kuu.

Ilikuwa ni krosi ya Ezekia Mwashilindi iliyomkuta Jeremiaha Juma ambaye aliunganisha, lakini kipa Beno Kakolanya aliokoa na mabeki wa Simba wakawa wazito kuondoa hatari hiyo, Asukile aliukuta, akageuka na kuujaza wavuni akihesabu bao pekee kwenye mechi hiyo.

Ni mechi ambayo wachezaji wa Simba hawakuwa kwenye kiwango kilichozoeleka, kwani pamoja na kuonekana kuwa wazito, lakini hawakuwa wakikaba na kuwaacha huru kwa muda mrefu Prisons kutawala, pia hakukuwa na shambulio kali la maana walilofanya.

Angalau mchezaji pekee aliyeonekana hatari, ni Denis Kibu (pichani chini) ambaye aliwekwa chini ya ulinzi mkali wa mabeki watatu wa Prisons, wakiwaacha wengine ambao hawakuwa na madhara.

Ni matokeo ambayo yameipandisha Prisons kutoka nafasi ya 15 hadi ya 14, ikifikisha pointi 29 na kuishusha Biashara United kwenye nafasi ya 15 na pointi zake 28. Simba imeendelea kubaki kwenye nafasi ya pili ikisalia na pointi 60 baada ya mchezo huo kumalizika kwa bao 1 - 0.

Hakuna timu iliyofanya shambulizi lolote la maana hadi dakika ya 18, Prisons ilipopiga hodi langoni mwa Simba kwa krosi ya Ibrahim Abraham iliyotaka kudakwa na kipa Beno Kakolanya, mpira ukamponyoka, Samson Mbangula akaupiga kwa kisigino kwa lengo la kuukwamisha wavuni, lakini Kennedy Juma alifanya kazi ya ziada akiwa katikati ya mstari wa goli akautoa ikawa kona.




9 770856 541002 >

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042